**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MKOA WA PWANI

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) YA MWAKA 2025 – 2030 KUANZIA JANUARI, 2026 HADI MACHI, 2026



**Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MKOA WA PWANI

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) YA MWAKA 2025 – 2030 KUANZIA JANUARI, 2026 HADI MACHI, 2026


**Imeandaliwa na:-**
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
2 Mtaa Wa Ishengoma
S.L.P 30080,
**61180 KIBAHA – PWANI**

**Simu Na.:** 255 23 240 2066
255 23 240 2287
**Barua pepe:** rc@pwani.go.tz


**JUNI, 2026**

# YALIYOMO


**1.0 UTANGULIZI ..... 1**

**2.0 UTEKELEZAJI KISEKTA WA MAELEKEZO MAHUSUSI NA MAELEKEZO YA JUMLA YA ILANI YA CCM ..... 1**

2.1. SEKTA YA KILIMO ..... 1

2.1.1. Kuimarisha Tija katika Kilimo: ..... 1

2.1.2 Utekelezaji uliofanywa na Serikali katika maelekezo ya jumla katika Sekta ya Kilimo ni kama ifuatavyo:– ..... 2

2.1.3 Mafanikio mengine yaliyopatikana katika sekta hii ya kilimo ni pamoja na;- ..... 3

2.2. SEKTA YA MIFUGO ..... 8

2.3. SEKTA YA UVUVI ..... 13

2.4. SEKTA YA MIUNDOMBINU ..... 15

2.4.1. Barabara ..... 15

2.4.2. Vivuko ..... 17

2.4.3. Utekelezaji wa Maelekezo ya Jumla kwenye sekta ya miundombinu (Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano) kama ifuatavyo: ..... 18

2.5. SEKTA YA NISHATI ..... 29

2.5.1. Mkoa umetekeleza maelekezo yaliyotamkwa kwenye ilani mahususi kwa Mkoa wa Pwani katika sekta hii kama ifuatavyo; ..... 29

2.6. SEKTA YA MAJI ..... 39

2.6.1. Pamoja na kutekeleza Maelekezo Mahususi kwenye Serikali imetekeleza pia Maelekezo ya Jumla katika Sekta ya Maji Vijijini kama ifuatavyo:– ..... 39

2.6.2. Serikali imetatua kero ya upatikanaji wa Maji kupitia Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) kama ifuatavyo: – ..... 42

**3.0 UTEKELEZAJI WA ILANI YA CCM KISEKTA KATIKA MAENEO MENGINE YENYE MAELEKEZO YA JUMLA ..... 43**

3.1. SEKTA YA VIWANDA ..... 43

3.2. SEKTA YA TEHAMA ..... 49

3.3. SEKTA YA ELIMU ..... 50

3.4. SEKTA YA AFYA ..... 54

3.5. SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII ..... 64

3.5.1. Utoaji wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ..... 64

3.5.2. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III) ..... 65

3.6. UKUSANYAJI WA MAPATO ..... 66

3.6.1. Ukusanyaji Wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania Mkoa wa Pwani (TRA - Pwani) ..... 66

3.6.2. Mapato ya Ndani ya Halmashauri ..... 66

3.7. SEKTA YA MICHEZO ..... 67

3.7.1 Kudumisha Utamaduni wa Taifa, na Kukuza Sanaa na Michezo ..... 67

3.8. SEKTA YA UTAWALA BORA NA UTAWALA WA SHERIA ..... 68

**4.0 HITIMISHO ..... 70**

# 1.0 UTANGULIZI

Mkoa wa Pwani unaendelea na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2025 na utekelezaji wake unaanzia mwaka 2025 – 2030 ambayo inalenga kuleta maendeleo kwa Wananchi wa Mkoa wa Pwani na Taifa kwa ujumla. Mkoa unatekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha malengo yaliyo kwenye Ilani yanatekelezwa ipasavyo. Kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2026 hadi Machi, 2026 Mkoa na utetekelezaji miradi yenye maelekezo mahususi yaliyotajwa kwenye Ilani ya Chama, maelekezo ya jumla na maelekezo ya ziada katika Sekta za Maji, Elimu, Afya, Kilimo, Ushirika, Viwanda na Biashara, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, Uchumi wa Buluu, Nishati, Maendeleo ya Jamii, Usafirishaji na Uchukuzi, na Utawala Bora. Mkoa umepata mafanikio makubwa katika Ilani ya CCM kama ifuatavyo: –

# 2.0 UTEKELEZAJI KISEKTA WA MAELEKEZO MAHUSUSI NA MAELEKEZO YA JUMLA YA ILANI YA CCM

Mkoa umeendelea na utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya CCM katika sekta mbalimbali zenye maeneo yaliyo na maelekezo Mahususi kwa Mkoa wa Pwani na yale ya Jumla kama ifuatavyo: –

## 2.1. SEKTA YA KILIMO

### 2.1.1. Kuimarisha Tija katika Kilimo: –

**Ibara ya 25 (e) na (f): Kuimarisha Tija katika Kilimo; Kwa Kuongeza Skimu za umwagiliaji na Kuongeza maeneo ya umwagiliaji. Kujenga Skimu ya Umwagiliaji ya Hekta 54,997 kwa kutumia fursa ya Bwawa la Nyerere na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani.**

Tume ya Umwagiliaji imefanya usanifu wa awali katika eneo lote chini ya Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa ajili ya kujenga skimu za umwagiliaji na matumizi mengine ambapo hadi sasa usanifu umefikia asilimia 90. Kwa upande wa Kilimo cha umwagiliaji, hatua ya upembuzi yakinifu imekamilika na hekta 64,200 zimepimwa tayari kuanza kuwekewa miundombinu ya umwagiliaji.

Aidha, Usanifu na upembuzi yakinifu umeshakamilika kwenye eneo lenye hekta 8,000 katika Kata ya Mtunda kwenye skimu ya Mbakiamturi na hekta 3,000 katika Kata ya Ngorongo ambapo mradi hii ipo katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya kuanza ujenzi. Skimu ya Chama cha Umwagiliaji cha Ruvu (CHAURU) Mkandarasi amepatikana, yupo site anaendelea na zoezi la mapitio ya michoro (design review) na Bwawa la Bagamoyo lipo katika hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu.

**2.1.2. Utekelezaji uliofanywa na Serikali katika maelekezo ya jumla katika Sekta ya Kilimo ni kama ifuatavyo:–**

**Ibara ya 25 (f): Kuanzisha mashamba makubwa kwa ajili ya kilimo cha pamoja na cha kisasa (block farming) kwa mazao ya kimkakati na yenye mahitaji makubwa nchini.**

Serikali imeanzisha Kilimo cha pamoja cha mazao ya Michikichi na Ufuta katika Halmashauri za Kisarawe na Rufiji. Jumla ya ekari 78,000 (Kisarawe ekari 38,000 na Rufiji ekari 40,000) za michikichi zimepandwa. Jumla ya ekari 500 zimetengwa kwa ajili ya kilimo cha ufuta ambapo kati ya hizo ekari 300 zimegawiwa kwa vijana 150 kulima ufuta katika Halmashauri ya Kisarawe.

Aidha, Bodi ya Korosho imepewa eneo kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha pamoja (ekari 6,500) kwa zao la Korosho Wilayani Rufiji. Hadi kufikia Machi, 2026 ekari 150 kati ya 6,500 zilizopo zimesafishwa kwa ajili ya kupanda mikorosho mipya.

Serikali imetenga eneo la ekari 2,000 kwa ajili ya kuwawezesha Vijana na Wanawake kupitia mradi wa Build Better Tomorrow (BBT) katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha (Lukenge ekari 1,600 na Lupunga ekari 400). Upimaji wa Afya ya udongo umefanyika na unafaa kwa kilimo na tayari Serikali imewapatia Wakulima matrekta mawili (2). Aidha, ekari 53 kati ya ekari 400 katika eneo la Lupunga zimesafishwa kwa ajili ya kilimo cha ufuta.

Kuanzisha kilimo cha Mbogamboga Kata ya Kikongo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 200. Kwa sasa upembezi yakinifu unaendelea.

**Ibara ya 25(a): Kuongeza upatikanaji wa mbegu bora na kwa bei nafuu yenye ukinzani dhidi ya magonjwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa iliyo salama kwa afya ya Watanzania katika mazao ya Kahawa, Michikichi, Migomba, Mihogo, Viazi, Minazi, Katani, Nanasi na Pareto;-**

Kwa msimu wa 2025/26 miche bora ya chikichi 60,000 imesambazwa na kupandwa na wakulima (Kisarawe miche 10,000, Mkuranga miche 30,000 na Kibiti miche 20,000). Aidha, msimu wa 2024/2025 mbegu bora za Chikichi miche 70,000 zilisambazwa kwa wakulima (Kibiti miche 30,000, Rufiji miche 10,000 na Bagamoyo miche 30,000).

**Ibara ya 25 (b), (c) na (d): Kuongeza usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na mbegu bora, mbolea, viuatilifu na zana bora za kilimo.**

i. Usambazaji wa mbolea za ruzuku msimu wa 2025/2026 unaendelea ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 jumla ya tani 8,040 za mbolea zimesambazwa katika Halmashauri mbalimbali;

ii. Usambazaji wa lita 50,454 (Mkuranga lita 20,517, Kibiti 21,826 na Rufiji 8,111) za pembejeo za kudhibiti wadudu kwenye maeneo ambayo korosho zinachipua mapema;

iii. Kusajili wakulima 26,800 (Kibaha 502, Kibaha Manispaa 56, Bagamoyo Mji 470, Kisarawe 1,236, Mkuranga 11,321, Kibiti 7,659, Rufiji Mji 4,702, Chalinze 796 na Mafia 56) kwa ajili ya kugawiwa pembejeo za korosho.

**Serikali imetekeleza vizuri Ibara ya 25 (g) ya Ilani ya CCM inayolenga kuongeza uzalishaji na tija kwa mazao ya chakula na biashara;-**

Mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili ni pamoja na:–

i. Kuongezeka kwa tija ya uzalishaji wa Mahindi kutoka Tani 1.7 mwaka 2024/2025 hadi Tani 3 mwaka 2025/2026;

ii. Tija ya uzalishaji wa Mpunga imeongezeka kutoka Tani 3.0 mwaka 2024/2025 hadi Tani 8.0 mwaka 2025/2026;

iii. Tija ya zao la Muhogo imeongezeka kutoka Tani 8 mwaka 2024/2025 hadi Tani 11 mwaka 2025/2026;

iv. Tija ya uzalishaji wa zao la Pamba limeongezeka kutoka Tani 0.4 mwaka 2024/2025 hadi Tani 0.5 mwaka 2025/2026;

v. Tija ya uzalishaji wa Ufuta umeongezeka kutoka Tani 0.3 mwaka 2024/2025 hadi Tani 1 kwa mwaka 2025/2026.

### 2.1.3. Mafanikio mengine yaliyopatikana katika sekta hii ya kilimo ni pamoja na;-

**Kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika kilimo cha kisasa cha kibiashara hususani ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na kuwashirikisha wakulima kwa kila mwaka.**

Uwekezaji wa kilimo cha kibiashara cha mashamba makubwa ya Miwa unaendelea kupitia makampuni ya Bagamoyo Sugar yenye ukubwa Hekta 10,000 kati ya hizo hekta 2,682 zimepadwa miwa kati 6,000 zinazofaa kwa kilimo cha miwa. Uzalishaji wa miwa kwa ajili ya kuchakata sukari ni tani 145 - 150 kwa hekta.

Shamba la Lake Agro la kilimo cha miwa lililopo Wilayani Rufiji lenye ukubwa wa hekta 16,000 ambapo kati ya hizo hekta 1,660 zimepandwa. Kwa sasa, ujenzi wa kiwanda cha kuchakata sukari unaendelea, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ikijumuisha mabwawa, vituo vya kusukuma maji, mabomba na mifereji ya kusafishia maji, mifumo ya umeme mkubwa, ujenzi wa nyumba za wafanyakazi na miundombinu ya barabara za mashambani unaendelea. Kiwanda kinatarajia kukamilika Oktoba, 2026 na kuanza kazi Novemba, 2026.

Aidha, katika kuendeleza kilimo cha ndizi Kampuni ya Food Star Trading Tanzania Limited iliyopo katika Halmashauri ya Mji Rufiji imesafisha eneo la hekta 1,000 kati ya hekta 6,600 kwa ajili ya kupanda migomba na ambapo hadi sasa hekta 20 za majaribio. Kampuni hii itakapoanza uzalishaji kamili itaajiri wafanyakazi 10,000 na kusafirisha makasha (container) 50 za ndizi kwa siku. Kwa sasa kampuni ipo kwenye hatua ya ujenzi wa maabara kwa ajili ya kuotesha miche kwa kwa ajili ya mbegu (tissue culture), ujenzi wa kituo cha kuhifadhi ndizi baada ya kuvuna kwa ajili ya kusafirisha na kuchimba mtaro wa kuchukua maji kutoka mto Rufiji hadi shambani ambapo hadi kufikia mwezi mei uchimbaji wa mtaro utakuwa umekamilika.

**Kuendelea Kuimarisha usimamizi wa huduma za ugani kwa kutumia TEHAMA kwa kuanzisha kituo cha huduma kwa wakulima (Call Center) na Maafisa Ugani kujengewa uwezo, mfumo utakaohakikisha wakulima wanafikiwa na changamoto zao zinazowakabili zinajibiwa kwa wakati.**

Serikali imesajili kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa eKilimo jumla ya Maafisa ugani 398 na wakulima 89,120. Mfumo huu humsaidia mkulima kuuliza maswali kwa njia ya simu na kujibiwa na wataalamu. Aidha, Wakulima wanapimiwa afya ya udongo kwa kutumia vifaa maalum kama vipima afya ya udongo ambavyo husaidia kutambua afya ya udongo ikiwemo virutubisho vinavyohitajika, aina ya mazao ya kupanda na aina ya mbolea ya kuongeza katika udongo.

### 2.1.3.1. Ushirika

**Ibara ya 25 (i): Kuimarisha vyama vya ushirika kwa kuhakikisha kuwa vyama vikuu vya ushirika vinatekeleza majukumu na kuvihudumia vyama wanachama wake kwa kusimamia uzalishaji, upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani, masoko na kuajiri watendaji wenye sifa kwa kuzingatia ukubwa wa chama na miamala inayofanywa ili kuongeza ufanisi na usimamizi katika Vyama vya Ushirika.**

Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa Pwani (CORECU Ltd) kimeendelea kuhudumia vyama wanachama na wakulima kwa kufanya yafuatayo:-

i. Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU LTD) na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) walisambaza mbegu bora za ufuta tani 12 (CORECU tani 6 na COPRA tani 6).

ii. Kutoa ajira kwa wataalam 78 wenye sifa katika sekta ya Masoko, Uhasibu na Ukarani, wanaotoa huduma ikiwa ni pamoja kutoa huduma za ugani na malipo kwa wakulima na wadau wengine.

iii. CORECU (1984) Ltd imegawa vipima unyevu ishirini (40) kwenye Vyama vya Ushirika vya msingi (AMCOS) kwa ajili ya kuongeza udhibiti wa ubora wa mazao yanayouzwa kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.

iv. Kusambaza mizani 188 za kidijitali katika vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS).

**Ibara ya 25 (g): Kuimarisha tija katika kilimo kwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao ya biashara; –**

CORECU Ltd imeendelea kusimamia minada ya Korosho, Ufuta na Mbaazi kupitia Mfumo wa Stakabadhi za ghala na kupata mafanikio yafuatayo:–

i. Kuongezeka kwa mauzo ya ufuta kutoka tani 13,053 yenye thamani ya TZS. bilioni 48.35 mwaka 2024/2025 hadi tani 27,475.5 yenye thamani ya TZS. bilioni 76.938 mwaka 2025/2026;

ii. Kuongezeka kwa uzalishaji wa korosho kutoka tani 25,862 msimu 2024/2025 hadi tani 35,153.80 msimu wa 2025/2026. Aidha, Mauzo ya korosho kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani na soko la awali yameongezeka kutoka tani 21,622 yenye thamani ya TZS. Bilioni 70.09 msimu wa 2024/2025 hadi tani 22,073.6 yenye thamani ya TZS. Bilioni 58.3 msimu wa 2025/2026. Kushuka kwa mapato kunatokana na kushuka kwa wastani wa bei kutoka shilingi 2,700 msimu wa 2024/2025 hadi shilingi 2,100 msimu wa 2025/2026.

iii. Kuongezeka kwa mauzo ya zao la Mbaazi kutoka tani 298.65 yenye thamani ya TZS. milioni 575.81 mwaka 2024/2025 hadi tani 959.69 yenye thamani ya TZS. milioni 973.54 mwaka 2025/2026.

**Ibara ya 25 (i): Kuimarisha vyama vya ushirika kwa kuongeza mikopo na idadi ya wanachama katika Vyama vya Ushirika kwa kuanzisha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOs) kwenye Ushirika wa Mazao na Masoko (AMCOS) na aina nyingine za vyama vya ushirika (Integrated Cooperatives).**

Katika Vyama vya Ushirika akiba imeongezeka kutoka TZS. bilioni 11.79 mwaka 2025 hadi TZS. bilioni 12.3 Machi, 2026. Mikopo imeongezeka kutoka TZS. bilioni 14.34 mwaka 2025 hadi TZS. bilioni 15.7 machi, 2026;

**Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na;-**

**i. Kuendelea kuimarisha elimu na mafunzo ya ushirika kwa wanachama, viongozi na watendaji kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika.**

Serikali kupitia Kamati ya Elimu ya Mkoa imeendelea kutoa elimu ya dhana ya Ushirika na kuhamasisha uanzishaji na uendelezaji wa vyama vya ushirika, ambapo jumla ya Watu 4,308 (Wanaume 2,817 Wanawake 1,491) wamepatiwa elimu.

**ii. Kuendelea na kuboresha uongozi, kudhibiti wizi na ubadhirifu ndani ya vyama vya ushirika kwa kuhimiza uzingatiaji wa kanuni za maadili ndani**

**ya vyama vya ushirika na kusisitiza matumizi ya mfumo wa TEHAMA ili kuimarisha usimamizi na upatikanaji wa takwimu sahihi.**

a. Kusimamia matumizi ya Mizani za kidigitali ambazo zitatumika kupima mazao ya wakulima, kutoa stakabadhi na kutunza kumbukumbu/taarifa za mazao ya wakulima ambapo hadi kufika machi, 2026 jumla ya mizani ya kidigitali 183 imegawiwa kwenye AMCOS 105; na

b. Kuimarika kwa matumizi ya Mfumo wa kidijitali wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) katika minada ya zao la Korosho, Ufuta na Mbaazi ambapo mfumo huo unatoa fursa kwa wanunuzi, wakulima na wadau mbalimbali kufuatilia minada ya mazao mubashara kupitia Kompyuta au simu janja.

iii. **Kuendelea kupanua wigo katika ushirika kwa kuhamasisha makundi maalum wakiwemo vijana, wanawake, mama lishe, bodaboda, watu wenye ulemavu, wazee n.k, kujiunga na kuanzisha vyama vya ushirika vinavyogusa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.**

Mkoa umefanikiwa kuanzisha vyama vya ushirika vya makundi maalumu vifuatavyo:-

a. Chama cha Ushirika cha Vijana Mafundi Seremala (Seremala Cooperative Society) chenye wanachama 78 (wanaume 50 wanawake 28) katika Kata ya Ikwiriri kwa ajili ya kuwajengea uwezo mafundi hao ili kupata mikopo na kutafuta masoko yenye tija.

b. Chama cha Ushirika cha “Survival Women” chenye wanachama 33 kinachojihusisha na kilimo cha mwani, mbogamboga na ufugaji wa jongoo bahari Wilayani Bagamoyo.

c. Chama cha Ushirika cha Vijana Mafundi Maboti (CHAMABOMA) chenye wanachama 23 (wote wanaume) kinachojihusisha na utengenezaji wa boti na uvuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

#### 2.1.3.2. Maliasili

Mkoa wa Pwani una jumla ya Misitu 99 yenye eneo la hekta 542,591.4. Kati ya Misitu hiyo, Misitu 30 yenye eneo la hekta 222,228 ipo chini ya usimamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS); Misitu 15 yenye eneo la hekta 88,960.6 ipo chini ya usimamizi wa Halmashauri na Misitu 52 yenye eneo la hekta 231,402.8 ipo chini ya usimamizi wa Serikali za Vijiji.

#### 2.1.3.3. Misitu na Nyuki

**Ibara ya 32 (a): Kuendeleza programu mbalimbali za upandaji miti, utunzaji na ukuzaji wa miti katika kila Halmashauri:**

i. Idadi ya miti iliyopandwa kwa mwaka 2025/2026 hadi kufika Machi, 2026 15,602,208 sawa na asilimia 115.57 ya lengo la upandaji miti 13,500,000 kwa Mkoa. Aidha, zoezi hili la upandaji miti ni endelevu.

ii. Mkoa unaendelea kusimamia na kuhamasisha matumizi ya Nishati safi kwa taasisi zinazolisha zaidi ya watu mia moja (100) ambapo mpaka sasa jumla ya Taasisi 140 kati ya taasisi 543 zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa wakati mmoja zinatumia nishati safi ya kupikia, sawa na asilimia 18.8. Uhamasishaji unaendelea.

### 2.1.3.4. Utalii

**Ibara ya 31 (a) – (b): Kuimarisha sekta ya utalii ili ili kuongeza watalii wa ndani na nje pamoja na kuongeza mapato yanayotokana na shughuli za utalii.**

Mkoa wa Pwani una jumla ya Vivutio vya utalii **87** vinavyojumuisha Mambokale, Misitu ya Hifadhi ya Mazingira Asilia, Mapori ya Akiba ya Selous na WamiMbiki, Hifadhi za Taifa za Nyerere na Saadani na Fukwe nzuri za Bahari. Katika kipindi cha 2025 - 2030 Mkoa umepata mafanikio mbalimbali katika Sekta za Wanyamapori na Utalii kama ifuatavyo:-

i. Kutoa elimu kuhusu uhifadhi wa wanyamapori na wanyama waharibifu na kufanya doria za kudhibiti maeneo ya ndani na nje ya hifadhi za Jumuiya ya Wanyamapori, Mapori ya Akiba na Hifadhi za Taifa.

ii. Kupandisha hadhi Hifadhi ya Jumuiya ya Wanyamapori (WMA) ya Wamimbiki kuwa Pori la Akiba la Wamimbiki ili kuongeza tija katika Utalii wa Uwindaji (Hunting Tourism).

iii. Kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka watalii 193,400 mwaka 2024 hadi watalii 265,117 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 37.08 na kuongeza mapato yatokanayo na utalii kutoka TZS. 21,027,879,000 kwa mwaka 2024 hadi TZS. 24,462,483,781 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 16.33

iv. Kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa hoteli za kitalii katika maeneo yafuatayo:-

   a) Wilaya ya Mkuranga (Palacha ekari 284);

   b) Mafia (Visiwa vya Mabarakuni na vinginevyo);

   c) Halmashauri ya Chalinze (Natasha na Dibangala kwenye Pori la Akiba la WamiMbiki na Uvinje, Mlima dumi, Mabumo na Forodha Ulaya kwenye Hifadhi ya Taifa ya Saadani), na

   e) Rufiji – Hifadhi ya Mwalimu Nyerere (Makubi, Kinyanguru I, II na III).








*Uwanja mpya wa Ndege katika Mbuga ya Wanyama ya Mwl. Nyerere Rufiji Mkoani Pwani*

## 2.2. SEKTA YA MIFUGO

**Mkoa umetekeleza maelekezo mahususi yaliyotamkwa kwenye ilani kwa Mkoa wa Pwani katika sekta ya Mifugo kama ifuatavyo: –**

**Ibara 26; Kuimarisha ufugaji wa kisasa;**

Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kwa kuboresha ranchi tano (Kongwa, Ruvu, Kalambo, Missenyi na West Kilimanjaro) ili kuongeza tija katika mnyororo wa thamani ya mazao ya mifugo. Aidha, sekta binafsi na wafugaji mmoja mmoja watahimizwa kuendelea kumiliki na kuboresha miundombinu katika ranchi zao ili kuwa na ranchi za kisasa ndani ya serikali na pia kwa wafugaji binafsi.

Serikali imeendelea kuimarisha Ranchi ya Ruvu kwa kuchukua hatua zifuatazo:–

i. Kukarabati malambo matatu (3), kuchimba kisima kirefu kimoja (1), kununua trekta moja (1) pamoja na mashine (mower, bailer, na raki) za kuvuna malisho.

ii. Kununua madume bora 20 ya mbegu aina ya boran kwa ajili ya kuboresha kosaafu za mifugo.

iii. Kutatua mgogoro wa ardhi wa muda mrefu kati ya Ranchi ya Ruvu na wananchi waliovamia. Mgogoro huu ulitatuliwa kupitia Kamati ya Mawaziri wa Kisekta, ambapo Serikali imemega jumla ya hekta 2,208 sawa na ekari 5,520 kwa Vijiji 10 vinavyozunguka Ranchi hiyo katika Halmashauri za Chalinze ekari 3,720 (Ruvu Darajani 500, Kidogozero 500, Kitonga 1,200, Milo 1,000, Magulumatali 500 na Vigwaza 20), Bagamoyo ekari 300 (Mkenge 100, Fukayosi 100 na Kidomole 100) na Kibaha ekari 1,500 (Mperamumbi). Maeneo ni kwa ajili ya matumizi ya makazi, kiuchumi na huduma za kijamii. Hatua inayoendelea sasa ni kuondoa wavamizi walioko ndani ya eneo la ranchi na kuongeza alama za mipaka zinazoonekana kwa urahisi.

iv. Kuondoa wananchi wavamizi katika maeneo ya kimkakati ya Ranchi ya Ruvu.

v. Aidha, wafugaji Nane (08) wamehimizwa kumiliki na kuboresha miundombinu katika ranchi zao akiwemo Ranchi ya 4G, Mbogo, Lushu, Lonhambi, Athumani, Lekonyori, Lisesi na Susa, ambao wamejenga lambo moja (1), kuchimba visima virefu viwili (02), kununua madume bora ya mbegu ya ng'ombe wa nyama 20, kulima malisho bora ekari 500, kujenga majosho manne (4) na vibanio viwili (2) kama ilivyoneshwa katika jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Maeneo yaliyofanyiwa maboresho katika Ranchi Ndogo**

| NA | HALMASHAURI | MAENEO YALIYOFANYIWA MABORESHO KWENYE RANCH BINAFSI | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Ranchi** | **Lambo** | **Visima virefu** | **Majosho** | **Malisho (ekari)** | **Vibanio** | **Madume ya mbegu** |
| 1 | Kibiti | 4G Ranch | - | 1 | 1 | - | - | - |
| 2 | Kibiti | Lekonyori Ranch | - | 1 | - | 10 | - | - |
| 3 | Chalinze | Mbogo Ranch | - | - | 2 | 0 | 2 | 10 |
| 4 | Kisarawe | Lushu Ranch | - | - | - | 120 | - | 5 |
| 5 | Kisarawe | Lohambi Ranch | - | - | - | 80 | - | 5 |
| 6 | Kisarawe | Athumani Ranch | 1 | - | 1 | 200 | - | - |
| 7 | Rufiji | Lisesi Ranch | - | - | - | 60 | - | 0 |
| 8 | Rufiji | Susa Ranch | - | - | - | 30 | - | - |
| | **JUMLA** | | **1** | **2** | **4** | **500** | **2** | **20** |

Ranchi hizi zimekuwa chanzo kizuri cha nyama bora, mbegu bora za ng'ombe na sehemu ya kujifunzia kwa wafugaji wa asili katika Mkoa.



*Picha ya juu inaonyesha ng'ombe bora kutoka Ranchi ya Mbogo–Ubena, Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze*

**Pamoja na utekelezaji wa maelekezo mahsusi yaliyotajwa kwenye ilani kuhusiana na Sekta ya Mifugo, Mkoa pia umefanya utekelezaji wa shughuli zifuatazo;**

**Ibara ya 26 (d): Kuongeza maeneo ya malisho na upatikanaji wa huduma za ugani kwa wafugaji kupitia mashamba darasa.**

Kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 jumla mashamba darasa 15 ya malisho yameanzishwa katika Halmashauri za Mkuranga 4, Rufiji 4, Kibaha 3, Kibiti 2 na Kisarawe 2. Aidha, jumla ya tani 84.84 za mbegu za malisho aina ya Junkao zimezalishwa kupitia shamba la mbegu za malisho la Vikuge, ambapo tani 13.41 ziligawiwa kwa wafugaji 20 katika Halmashauri za Wilaya za Kisarawe (5), Chalinze (5), Kibaha (3), Mkuranga (3), Kibiti (2), Rufiji (2) na kupandwa kwenye maeneo yenye jumla ya ekari 41.

**Ibara ya 26 (e): Kuongeza na kuimarisha ujenzi wa machinjio ya kisasa katika maeneo yote Halmashauri.**

i. Machinjio ya kisasa yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 1,500 na mbuzi na kondoo 2,000 kwa siku imejengwa na Kampuni ya Union Meat Abattoirs Ltd katika Kijiji cha Ruvu Darajani Halmashauri ya Chalinze. Uchinjaji umeanza na nyama inayozalishwa inauzwa katika nchi za Qatar, Saudi Arabia na Dubai.

ii. Serikali inaendelea na usimamizi wa machinjio nyingine za Manispaa ya Kibaha iliyopo eneo la Pangani na TANCHOICE iliyopo Soga, Halmashauri ya Kibaha ili ziendelee kutoa nyama bora kwa ajili ya masoko ya ndani na nje sawia.

**Ibara ya 26 (b) na (c): Kujenga na kukarabati majosho kwa ajili ya kuogesha mifugo na mabwawa kwa ajili ya kunyweshea maji mifugo.**

Ujenzi wa majosho mawili (2) umekamilika katika Halmashauri ya Wilaya Kisarawe na josho moja katika Halmashauri ya Mji Bagamoyo. Mifugo imeogeshwa kwa kufanya michovyo 2,051,078 ya ng'ombe, 1,270,549 ya mbuzi na 270,053 ya kondoo. Aidha, dozi za chanjo za mifugo dhidi ya magonjwa mbalimbali zimetolewa kwa ng'ombe 245,174, mbuzi na kondoo 113,250, kuku 3,152,016.00, mbwa 12,261 na paka 710.


Wizara ya Mifugo imejenga lambo moja (1) la maji katika Kijiji cha Vinyeze Halmashauri ya Wilaya Kibaha na kuchimba kisima kirefu katika Kijiji cha Matanzi Halmashauri ya Wilaya Mkuranga.


**Ibara ya 26 (a): Kuimarisha ufugaji wa kisasa kwa kutenga, kupima na kumilikisha maeneo kwa wafugaji**;


Mkoa umetekeleza Mpango wa ranchi ndogo ambapo jumla ya Ranchi ndogo 847 (Kibiti 363, Rufiji 371, Chalinze 2, Kisarawe 70 na Mkuranga 41) kwenye eneo la ukubwa wa jumla ya hekta 38,319.97. Wafugaji 952 wenye Mifugo 86,278 wamepangwa kwenye ranchi hizo. Aidha, Wafugaji 321 (Rufiji 161, Kibiti 136 na Kisarawe 24) wamepata hati za kimla za umiliki wa ardhi. Upangaji huu umesaidia kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji kutoka asilimia 97 mwaka 2020 hadi asilimia 52 mwaka 2026.



*Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2026 Ndg. Wazo Michael Mwang'onda akikabidhi hati ya kimila kwa mmoja wa wafugaji walio rasimishwa maeneo ya ufugaji katika Halmashauri ya Mji Rufiji*


RAMANI YA WILAYA YA RUFIJI INAYO ONESHA MAENEO YA RANCHI NDOGO MACHI 2026
Nyerere National Park
Selous Game Reserve
Wilaya ya Kibiti
BAHARI YA HINDI
Mkoa wa Lindi
Mloka
FUNGUO
Ranchi ndogo
Barabara
Kijiji
Wilaya
Vyanzo vya maji
;Drawn by japhet JM


RAMANI YA RANCHI NDOGO ZA KIJIJI CHA CHUMBI C
WILAYA YA RUFIJI - MKOA WA PWANI 2026
MTO KIHENGEA
ENEO LA AKIBA CHUMBI C
ENEO LA AKIBA CHUMBI C
ENEO LA MAKAZI
3,821 EKARI JUMLA
58 RANCHI JUMLA
SCALE 1:20000
TO LINDI
LISESI RANCHI
RANCHI NAMBA 2
107 EKARI
RCR 60
RCR 61A
RCR 61
RCR 61B
RCR 62A
RCR 62
RCR 79
RCR 63
RCR 64
RCR 67
693
700
466
302
259
TO LINDI




Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa Mpango wa Ranchi Ndogo Mkoani Pwani

| Na. | H/shauri | Idadi ya Vijiji | Eneo lililoendelezwa (Ha) | Idadi ya vitalu/ kongani | Idadi ya wafugaji waliopangwa | Idadi ya Mifugo iliyopangwa kwenye Ranchi | Idadi ya Hatimiliki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kibiti | 14 | 12,851.20 | 363 | 380 | 38,975 | 136 |
| 2 | Rufiji | 8 | 11,542 | 371 | 334 | 25,999 | 161 |
| 3 | Chalinze | 6 | 2,567.84 | 2 | 203 | 13,213 | 0 |
| 4 | Kisarawe | 2 | 9,846 | 70 | 35 | 8,091 | 24 |
| 5 | Mkuranga | 4 | 1512.93 | 41 | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **34** | **38,319.97** | **847** | **952** | **86,278** | **321** |

## 2.3. SEKTA YA UVUVI

**Kuendelea kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia ya uvuvi endelevu ili iweze kuhimili ushindani na kuifanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya samaki na kuachana na uagizaji kutoka nje. Pia kuzalisha ajira nyingi zaidi kwa vijana na kuboresha maisha ya wavuvi na wananchi kwa ujumla. Mkoa umetekeleza yafuatayo: –**

i. Uzalishaji wa samaki baharini umeongezeka kutoka tani 7,849 hadi kufikia tani 17,507 sawa na ongezeko la asilimia 123.05 huku uzalishaji katika mabwawa ukiongezeka kutoka tani 678 hadi tani 1,612;

ii. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mwani kutoka tani 711 hadi tani 1,334

iii. Kuanzisha shamba darasa la ufugaji wa samaki lenye mabwawa 4 ya thamani ya TZS. Milioni 169 katika Halmashauri ya Mkuranga;

iv. Kuwekaa mazingira bandia ya samaki baharini FAD (Fish Aggregatted Devive) unaotekelezwa na Programu ya AFDP katika Halmashauri ya Bagamoyo ambapo FAD 8 kati ya 10 zimeshawekwa baharini;

v. Usimamizi wa rasilimali za uvuvi umeendelea kuimarika kwa vikundi vya BMUs kutoka vikundi 12 hadi vikundi 49 Machi, 2026.

vi. Kutoa mikopo ya boti 31 kwa vikundi vya wavuvi, Makampuni na vyama vya wavuvi katika Halmashauri za Bagamoyo (3), Mkuranga (15), Kibiti (5) na Mafia (8) ili kuongeza tija kwenye shughuli za uvuvi na kilimo cha mwani. Pia tunatarajia kupokea boti nyingine 8 katika awamu ya pili kwenda kwa wanufaika katika Halmasahuri za Mkuranga(7) na Bagamoyo (1).

vii. UNDP kupitia Halmashauri ya Bagamoyo imekabidhi jumla ya vihori 13 (boti ndogo za kubebea mwani) ambavyo ni vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za ukulima wa mwani kwa vikundi 13. Vitendea kazi hivi vitagawiwa kwa vikundi ambavyo vinajishughulisha na ukulima wa mwani;

viii. Kuanzisha ufugaji wa Jongoo bahari hadi sasa ekari nane (8) zinatumika katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya kilo 612 zilivunwa. Malengo ya Mkoa ni kuongeza uzalishaji kutoka kilo 612 hadi 1,200 kwa mwaka. Aidha, ekari 36 (Bagamoyo ekari 10, Mkuranga ekari nane(8) na Mafia ekari 18) zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa jongoo bahari;

ix. Kukamilika kwa ujenzi wa Soko la Samaki la kisasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Kwa sasa wako maandalizi awamu ya pili ya ujenzi wa soko hilo.

x. Ili kulinda mazalia ya samaki, jumla ya mikoko 634,321 imepandwa katika Halmashauri za Mkuranga na Bagamoyo kufikia Machi 2026.



*Bwawa la Samaki Tanlapia Halmashauri ya Wilaya ya Mji Bagamoyo*



*Machinjio ya Union Meat Ruvu Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze*

## 2.4. SEKTA YA MIUNDOMBINU

**Mkoa umetekeleza maelekezo yaliyotamkwa mahsusi kwa Mkoa wa Pwani katika sekta ya Miundombinu (Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano) kama ifuatavyo: -**

**Katika kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji; Ibara 40 (a); Kuongeza mtandao wa barabara za lami za kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya kama ifuatavyo;**

### 2.4.1. Barabara

**i. Barabara ya Tanga – Pangani – Saadani – Bagamoyo (km 178);**

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami na daraja la Wami chini umekamilika. Ujenzi wa Barabara hii unaendelea kwa upande wa Tanga kwa ufadhili wa Benki ya maendeleo ya Afrika (ADB). Barabara ya Afrika Mashariki kuunganisha Mkoa wa Pwani na Tanga. Katika mradi huu unajengwa kwa sasa kuanzia Tanga hadi Mkange (km 90) ambapo urefu wa km 14 uko Mkoa wa Pwani. Mkandarasi anaendelea na ujenzi kwa upande wa Mkoa wa Tanga amefikia asilimia 46. Ujenzi wa km 74 kati ya Mkange - Makurunge utaanza baada ya taratibu za kibajeti kukamilika..

**ii. Barabara ya Kisarawe – Maneromango (Km 44 kati Km 54)**

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami imekamilika kwa km 54. Barabara hii ni kiungo muhimu na kuelekea Bwawa na Mbuga ya Mwalimu Nyerere. Hadi sasa jumla ya km 20 kati ya Kisarawe na Kisanga zimejengwa kwa kiwango cha lami. Sehemu ya barabara yenye urefu wa km 34.5 kuanzia Kisanga hadi Maneromango iko kwenye hatua za manunuzi ya Mkandarasi. Barabara hii ilihusisha Idadi ya Wafidiwa 958 kwa Kiasi TZS. bilioni 1.542

iii. **Barabara ya Makofia – Mlandizi – Vikumburu (Km 148)**

Barabara ya Makofia - Mlandizi – Vikumburu ni barabara ya Mkoa ambayo inaunganisha Wilaya ya Bagamoyo, Kibaha na Kisarawe. Ujenzi wa barabara hii yenye jumla ya urefu wa km 100 kwa kiwango cha lami unatekelezwa kwa awamu ambapo hadi sasa urefu mita 300 umejengwa enbeo la Mzenga. Hata hivyo urefu wa km. 15 kuanzia Mlandizi hadi makutano ya stesheni ya SGR ya Ruvu unatekelezwa katika mradi wa ujenzi wa barabara kuanzia Mlandizi hadi Stesheni ya Ruvu SGR Km. 23 ambapo utekelezaji wake upo katika hatua ya maandalizi. Barabara ilihusisha Idadi ya Wafidiwa 3036 kwa kiasi shiling bilioni 22.439. Jedwali la fidia limekwisha wasilishwa Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya maombi ya fedha

iv. **Barabara ya Kibaha – Mapinga (Km 23);**

Serikali imejenga barabara hii hadi sasa kwa urefu wa km 4.7 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya TZS. **6,547,776,567.50**. Ujenzi wa urefu uliobakia unatekelezwa kwa sehemu mbili kwa ghrama ya TZS. **23,922,846,731.11**: Sehemu ya kwanza kuanzia NIDA - Pangani (km 3.8) kwa gharama ya TZS. **5,628,737,395.00** ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 85 ukitarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2027. Sehemu ya pili kuanzia Pangani - Mapinga (km 14.5) kwa gharama ya TZS. **18,294,109,336.11** ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 13 akiwa amelipwa kiasi cha TZS. 1,694,909,822.50 ukitarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2027. Barabara ilihusisha Idadi ya Wafidiwa 293 kwa kiasi shiling bilioni 6.6136.

v. **Barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro (Km 210) kuwa njia nne (Express way):**

Mradi huu unatekelezwa kwa mfumo wa PPP (Public, Private Partnership) ambapo ujenzi unatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Usanifu wa awali wa mradi huu kuanzia Kibaha hadi Morogoro umeshafanyika. Utekelezaji wa mradi upo katika hatua ya manunuzi kwa sehemu ya Kibaha-Chalinze (Km 78).

vi. **Barabara ya Kilindoni – Ras Mkumbi (Km 52.3)**

Barabara ya Kilindoni - Rasimkumbi ina urefu wa km 52.28 na ujenzi wake umeendelea kwa awamu. Hadi sasa urefu wa km 2.15 kwa kiwango cha lami umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali imetenga kiasi cha TZS. **2,000,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi km 50.13 za barabara hii. Utekelezaji wake uko katika hatua ya Manunuzi ya Mkandarasi wa ujenzi. Marejeo ya mahitaji ya fidia yanaonyesha kwamba kiasi cha TZS. **8,415,213,000.00** kwa wananchi 1187 kinahitajika kwa ajili ya madai ya fidia. Jedwali la fidia limekwisha wasilishwa Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya maombi ya fedha.

vii. **Barabara ya Bungu – Nyamisati (Km 43)**

Barabara hii ikikamilika itarahisisha usafirishaji wa mizigo na abiria kuelekea Kisiwa cha Mafia kupitia bandari ya Nyamisati. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika Julai, 2024. Katika Mwaka wa fedha 2026/27

makisio ya ujenzi wa ujenzi wa kim.40.3 yamewasilishwa kwenye bajet kwa ajili kuidhinishwa. Utekelezaji utaanza mara baada ya taratibu za kibajeti kukamilika. Mahitaji ya fidia yanaonyesha kwamba kiasi cha TZS. **329,530,000** kwa wananchi 57 kinahitajika kwa ajili ya madai ya fidia.

**viii. Barabara ya Utete – Nyamwage (Km 33.7)**

Ujenzi wa barabara hii ulikuwa umeanza na km 0.3 pamoja na mzunguko wa Nyamwage kwa gharama ya TZS. Milioni 980. Hadi sasa zimejengwa jumla ya km1.55 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya TZS. bilioni 2.78. Aidha, kwa sasa ujenzi wa urefu wa km 32.15 uliobakia unajenga kwa gharama ya TZS. bilioni 43.419 na malipo ya awali ya TZS. bilioni 4.282 imelipwa kwa Mkandarasi sawa na asilimia 10. Mradi huu ulianza utekelezaji wake mnamo tarehe 26 Julai, 2023 na unatarajiwa kukamillika tarehe 30 Desemba, 2027 kulingana na Mkataba. Utekelezaji umefikia asilimia 17. Hadi sasa zoezi la ulipaji fidia kwa Wananchi 92 kwa kiasi cha TZS. 402,091,891.47 limekamilika.




*Ujenzi wa Barabara ya Utete - Nyamwage kwa kiwango cha Lami*

### 2.4.2. Vivuko

**Ibara 40 (i) na (j): Kujenga Vivuko vipya, kukarabati vilivyopo na miundombinu ili kuimalisha usalama na ubora wa huduma za usafirishaji;**

i. Ujenzi wa kivuko cha Nyamisati – Mafia - kivuko cha nyongeza umefikia asilimia 67. Ujenzi wa kivuko hicho unatekelezwa na Mkandarasi M/s KL Heavy Industry Company Limited ya Korea na Dar es Salaam Merchant Group Limited kwa gharama ya TZS. 9,499,118,530.76. Mkandarasi amelipwa asilimia 50.18 ya gharama kuu, vifaa kwa ajili ya ujenzi wa kivuko hiki vimefikishwa eneo la ujenzi na ujenzi unaendelea.




*Mchoro na picha ya kivuko kipya cha Nyamisati (Kibiti) - Kilindoni (Mafia) kinachojengwa Kimbiji jijini Dar es Salaam*

iii. Ujenzi wa maegesho ya Utete. Utafiti unaendelea kufanyika kutokana na jiografia ya mto Rufiji. Aidha, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/26 imetengewa kiasi cha TZS. 36,294,285.00

**2.4.3. Utekelezaji wa Maelekezo ya Jumla kwenye sekta ya miundombinu (Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano) kama ifuatavyo;**

**Ibara ya 40 (a), (b) na (c); Kuongeza mtandao wa barabara za lami, kufanya upanuzi na ukarabati mkubwa katika barabara na na kujenga barabara za lami zinazokwenda kwenye makazi ya watu, shughuli za biashara na maeneo ya biashara.**

**i. Kibaha – Mlandizi – Chalinze (Km 75)**

Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya Km 14.71 zimekarabatiwa kwa kuondoa tabaka la zamani liloharibika na kuweka tabaka jipya la lami liliboreshwa (SP 12.5).

ii. **Barabara ya Chalinze – Magindu – JNHPP – Utete (Km 354.9)**

Utekelezaji wa mradi kwa barabara hii unatokana na maelekezo ya Mheshimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 22 Disemba 2022 akiwa katika Sherehe za kuanza kujaza maji katika Bwawa la JNHPP. Utekelezaji wake uko katika hatua ya Usanifu wa Kina ambao unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/27 kwa gharama ya TZS. bilioni 1.7. Taarifa yake itawezesha Serikali kupata gharama za ujenzi na fidia. Mradi huu utahusisha ujenzi wa daraja la Utete (km1.0)

iii. **Ujenzi wa Daraja la Mbambe (M 81) pamoja na barabara Unganishi Km 3.**

Utekelezaji wa Mradi huu umeanza tarehe 18 Mei, 2023 na unatarajiwa kukamilika tarehe 12 Julai, 2027 ukigharimu kiasi cha TZS. 24,164,904,622.00 ambapo mpaka sasa Mkandarasi ameshalipwa malipo ya awali kiasi cha TZS. 6,199,601,556.01. Utekelezaji wa kazi uko asilimia 49.

iv. **Barabara ya Kiluvya – Mpuyani (Km 19.8)**

Barabara hii itaunganisha Wilaya ya Kisarawe na Makao Makuu ya Mkoa. Kazi ya upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina imekamilika Julai, 2024, hivyo itawezesha Serikali kupanga bajeti ya ujenzi. Zoezi la uhakiki wa uthamini wa mali za wananchi wanaopisha ujenzi wa barabara hii limekamilika, na Wananchi 152 walioathirika watafidiwa kwa kiasi cha TZS.15.496bio. Katika Mwaka wa fedha 2026/27 makisio ya ujenzi wa km.19.8 yamewasilishwa kwenye bajeti kwa ajili kuidhinishwa. Utekelezaji utaanza mara baada ya taratibu za kibajeti kukamilika.





*Ujenzi wa Daraja la Mbambe Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji*

v. **Barabara ya Mkuranga – Kisiju (Km 45)**

Barabara hii ikikamilika itarahisha usafirishaji kwenda/kutoka bandari ya Kisiju. Ujenzi wa km. 7.29 umekamilika kati ya Mkuranga Mjini hadi kijiji cha Msufini. Usanifu umekamilika mwezi Julai, 2024. Katika Mwaka wa fedha 2026/27 makisio ya ujenzi wa ujenzi wa km. 37.71 yamewasilishwa kwenye bajeti kwa ajili kuidhinishwa. Utekelezaji utaanza baada ya idhini ya kuanza ujenzi kutolewa. Barabara  hii itahusisha fidia kwa Wananchi 59 walioathirika watafidiwa kwa kiasi cha TZS. 512,822,000.00. Jedwali la fidia limekwisha wasilishwa Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya maombi ya fedha.

vi. **Barabara ya Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass) (Km 10)**

Barabara hii inaunganisha barabara kuu ya Morogoro eneo la Msolwa na barabara kuu ya Chalinze - Segera eneo la Msoga, Wilayani Bagamoyo, katika Halmashauri ya Chalinze. Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2022/23 na 2023/24 kwa ujumla imetenga kiasi cha TZS. 9,298,569,097.00 kwa ajili ya ukarabati wa Barabara hii. Kazi za ukarabati zinandelea kwa jumla ya km 6.7 kuanzia kwenye tabaka la udongo. Utekelezaji wa mradi uko asilimia 95. Aidha kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilitenga kiasi cha TZS. Bilioni 1.00 kwa ajili ya ukarabati wa urefu wa km 0.8 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 75. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetenga jumla ya kiasi cha TZS. bilioni 3.00 kwa ajili ya ukarabati wa urefu wa km 2.3 ambapo utekelezaji wake uko katika hatua za maandalizi. Miradi hii ikikamilika, jumla ya km 9.8 kati ya 10 zitakuwa zimekarabatiwa.

vii. **Barabara ya Mandera – Mkange – Saadani (Km 60)**

Barabara hii itaunganisha Barabara kuu ya Chalinze - Segera na Barabara mpya ya Afrika Mashariki katika eneo la Mkange na kuwezesha watalii kufika mbuga ya wanyama ya Saadani. Taarifa ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina itakamilika katika mwaka wa fedha 2026/27. Taarifa ya Usanifu itawezesha Serikali kupata gharama za ujenzi na fidia kwa ajili ya kupanga bajeti.

viii. **Barabara ya Mlandizi – Ruvu SGR (Km 23)**

Ujenzi wa barabara ya Mlandizi - Ruvu JCT - Ruvu SGR (km 23) utajumuisha ujenzi wa mzunguko eneo la Mlandizi (Roundabout). Mkandarasi atajenga barabara ya Mlandizi hadi Stesheni ya SGR ya Ruvu (km 23) ambapo urefu wa km 15 (Mlandizi-Makutano ya Stesheni ya Ruvu) ni sehemu ya barabara ya Mlandizi - Maneromango (km 65) na km 8 ni barabara ya Wilaya inayosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Pwani. Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya kiasi cha TZS. 60,250,755,910.00 kuanzia tarehe 14 Januari, 2026 na unatarajiwa kukamilika 12 Januari, 2028 kwa mfumo wa Sanifu - Jenga. Utekelezaji wake uko katika hatua za maandalizi (Mobilization).

ix. **Barabara ya Ikwiriri-Mkongo (km 30.74)**

Barabara hii ni kiunganishi cha Mikoa ya Kusini na nchi Jirani kwa kuwezesha watalii kufika kwenye Bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JHPP) na mbuga ya Wanyama ya Mwalimu Nyerere kupitia Ikwiriri mjini. Utekelezaji wa ujenzi wa sehemu ya Barabara ya km 27.74 zilizobaki upo katika hatua za manunuzi ya kumpata Mkandarasi. Barabara hii itahusisha fidia kwa Wananchi 1073 walioathirika watafidiwa kwa kiasi cha TZS. 4,823,433,935.03.

**x. Barabara ya Morogoro (Kibaha Mail moja-Picha ya ndege (km 3.6))**

Mradi wa upanuzi wa Barabara hii ni mwendelezo wa ujenzi wa TANZAM kuanzia Kimara hadi Kibaha kwa njia nane. Kazi ya Usanifu imekamilika katika mwaka wa fedha 2025/26. Katika Mwaka wa fedha 2026/27 makisio ya ujenzi wa km.3.6 yamewasilishwa kwenye bajeti kwa ajili kuidhinishwa. Utekelezaji utaanza mara baada ya taratibu za kibajeti kukamilika.



*Barabara ya Morogoro (Kibaha Mailimoja – Picha ya Ndege)*

**xi. Barabara ya Ubena JCT-Lugoba (km 30.75)**

Utekelezaji wake uko katika hatua za Usanifu wa Kina na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2026/27. Taarifa ya Usanifu itawezesha Serikali kupata gharama za ujenzi na fidia kwa ajili ya kupanga bajeti.

**xii. Barabara ya Maneromango – Vikumburu – Mloka-JNHPP (km 198.71)**

Utekelezaji wake uko katika hatua ya Usanifu wa Kina na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2026/27. Taarifa ya Usanifu itawezesha Serikali kupata gharama za ujenzi na fidia ili kupanga bajeti. Barabara hii itahusisha fidia kwa Wananchi 985 walioathirika watafidiwa kwa kiasi cha TZS. 1,542,534,798.72 na Jedwali la fidia limekwisha wasilishwa Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya maombi ya fedha

**xiii. Barabara zilizo pandishwa hadhi kuwa barabara za Mkoa**

Katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali imepandisha hadhi barabara zenye urefu wa km.106.1. Aidha Serikali imetenga kiasi cha TZS. 10,123,046,220.00 Kwa ajili ya ukarabati kwa kuzichonga, kuweka

changarawe na ujenzi wa kiwango cha lami, zege na daraja la boksi kalvati katika maeneo korofi. Aidha Katika mwaka wa fedha 2026/27, Serikali imepanga kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami na zege katika maeneo korofi.

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 40 (d) na (e) ya Ilani ya CCM yenye lengo la Kuimarisha TARURA kwa kuongeza bajeti ili kuendelea na ujenzi wa madaraja na vivuko vya zege na mawe pamoja na kuimarisha ukarabati wa barabara za changarawe kwa barabara za vijijini na mijini.**

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Pwani imepitishiwa bajeti ya jumla ya TZS. 29,489,691,827.81 kwa mwaka wa fedha 2025/26 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara katika mwaka wa fedha husika. Kati ya fedha hizo, TZS. 13,950,000,000 ni fedha za tozo, TZS. 4,275,000,000 ni fedha za jimbo, TZS. 6,904,691,827.81 ni fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo (RF), na TZS. 4,310,000,000.00 ni fedha za Mfuko wa Barabara maendeleo (RF). Fedha hizi zinajenga barabara za lami kilomita 3.96, barabara za changarawe kilomita 351.82, pamoja na kujenga miundombinu ya kupitisha maji ikiwemo kalavati mistari 231, maboksi ya kalavati 5, mifereji yenye urefu wa mita 43,380 na drifti 3. Aidha, fedha hizo zitatumika kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 966.27(RM, PM & SP).

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, TARURA Mkoa wa Pwani imesaini jumla ya mikataba 21 yenye thamani ya TZS. 7,231,730,500.00, utekelezaji wa kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara umefikia wastani asilimia 59 kwa ujumla, huku hatua za utekelezaji zikitofautiana kulingana na Wilaya. Aidha hadi sasa kiasi cha TZS. 1,131,160,000.00 kimeshalipwa sawa na asilimia 15.64 ya mikataba iliyoingiwa.

**Miradi ya Ilani ya CCM Iliyotekelezwa na TARURA kwa Kipindi cha 2025 – 2030.**

Sehemu hii inahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha mwaka 2025 – 2030 katika Halmashauri mbalimbali za Mkoa wa Pwani. Lengo la miradi hii ni kuboresha miundombinu ya barabara, mifereji ya maji ya mvua pamoja na miundombinu mingine muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika Halmashauri mbalimbali kama ifuatavyo;-

i. **Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha (Kibaha DC)**

Mradi wa ujenzi wa boksi kalavati katika barabara ya Kilangalanga–Mwanabito (km 10.71) unatekelezwa na Msoro Construction Company Limited kwa gharama ya TZS. 338,113,480 zinazotokana na fedha za Benki ya Dunia. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 99, hata hivyo bado

hakuna malipo yaliyofanyika kwa mkandarasi. Aidha, mradi wa Janga–Makazi Maoya umeingizwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya utekelezaji wake.



*Ujenzi wa Boksi Kalvati barabara ya Kilangalanga - Mwanabwito*

**ii. Halmashauri ya Manispaa Kibaha (Kibaha MC)**

Mradi wa ujenzi wa barabara ya Tughe – Anglican (km 1.1) pamoja na Picha ya Ndege – Lulanzi Hospitali – NDC (km 3.7) kwa kiwango cha lami unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) la Benki ya Dunia kwa gharama ya TZS. 19,832,922,855.99. Mkandarasi Dimetoclasa Real Hope Limited amelipwa malipo ya awali ya TZS. 2,974,938,428.399 na utekelezaji umefikia asilimia 9.5.

Mradi wa barabara ya Picha ya Ndege – Bokotimiza unatekelezwa kwa awamu mbalimbali kama ifuatavyo:

a. Mwaka 2022/2023: mita 700 zimekamilika kwa gharama ya TZS. 943,500,600;

b. Mwaka 2023/2024: mita 550 zimekamilika kwa gharama ya TZS. 759,185,000;

c. Mwaka 2024/2025: mita 520 zimefikia asilimia 95 ya utekelezaji kwa gharama ya TZS. 760 kwa mujibu wa mkataba na mpaka sasa mkandarasi ameshalipwa kiasi cha TZS. milioni 273 na ujenzi bado unaendelea; na

d. Mwaka 2025/2026: mita 650 zipo katika hatua ya kuanza utekelezaji.

Aidha, mradi wa barabara ya Kongowe Forest–Yombo (km 0.7) umefikia asilimia 95 ya utekelezaji, huku mradi wa Kwamfipa – Msangani (km 0.4) ukiwa umefikia asilimia 32.



*Ujenzi wa Barabara ya Picha ya Ndege - Sofu kwa Kiwango cha Lami Manispaa ya Kibaha*

**iii. Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti (Kibiti DC)**

Mradi wa ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 4.5 unaotekelezwa na Rabco Construction Ltd una thamani ya TZS. 1,962,641,263.13 na umefikia asilimia 60 ya utekelezaji.



*Ujenzi wa Mfereji wa Maji pamoja na Boksi Kalavati Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti*

iv. **Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe (Kisarawe DC)**

Mradi wa ujenzi wa boksi kalavati katika barabara ya Mzenga – Gwata unatekelezwa na Neloyt (T) Limited kwa gharama ya TZS. 359,670,000 na umefikia asilimia 70 ya utekelezaji.

v. **Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga**

Mradi wa ujenzi wa barabara ya Mkamba – Chamgoi (km 0.3) kwa kiwango cha zege unaotekelezwa na Link Construction Limited umefikia asilimia 50 ya utekelezaji.





*Barabara ya Kimanzichana - Chamgoi, Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga iliyojengwa kwa Kiwango cha Zege*

**vi. Halmashauri ya Mji Rufiji**

Katika Wilaya ya Rufiji, miradi mbalimbali inaendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na:-

a. Ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua Ikwiriri (km 10) umefikia asilimia 35;

b. Ujenzi wa barabara za lami Ikwiriri (km 20), ambapo km 10 zimekamilika; na

c. Ujenzi wa barabara za lami Utete (km 10), ambapo km 1 inaendelea.

Aidha, ujenzi wa Daraja la Mohoro unaotekelezwa na MAC Contractors Co. Ltd kwa gharama ya TZS. bilioni 17.85 umefikia asilimia 63 ya utekelezaji, huku jumla ya TZS. 7.43 bilioni zikiwa zimelipwa. Mradi unatarajiwa kukamilika tarehe 24 Machi 2026.

**vii. Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze**

Mradi wa ujenzi wa barabara za lami kilomita 4 katika mji wa Chalinze upo katika hatua yausanifu. Mradi wa dharura katika barabara ya Vigwaza – Mbuyuni unaotekelezwa na Higo Investment Company Limited umefikia asilimia 75 ya utekelezaji.

Aidha, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

a. Ujenzi wa boksi kalavati 2 katika barabara ya Mbwewe – Kikwazu;

b. Ujenzi wa barabara za changarawe km 2 (Vigwaza – Visezi – Ruvu); na

c. Ujenzi wa barabara za changarawe km 4 (Mboga – Diozile).

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 40 (f) na (g): ya Ilani ya CCM yenye lengo la kusimamia ujenzi wa bandari mpya ya bagamoyo na kuboresha bandari ya Kwala zilizopo katika Mkoa wa Pwani.**

**Mkoa kupitia Bandari ya Dar es salaam (TPA) imendelea na uendelezaji na ujenzi wa bandari zilizopo katika Mkoa wa Pwani kama ifuatavyo;-**

**i. Bandari ya Bagamoyo**

Uhuishaji wa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa Bandari Mpya ya Mbegani umekamilika. Mradi huu unapangwa kutekelezwa kwa awamu tatu na kwa sasa Serikali ipo katika hatua za kutafuta na kuhamasisha vyanzo vya fedha, ikiwemo ushiriki wa Sekta Binafsi, kwa ajili ya utekelezaji wake.

Aidha, maandalizi ya awali ya utekelezaji wa awamu ya kwanza yameanza, ambapo yatahusisha uchimbaji na uongezaji wa kina cha lango la kuingilia na kugeuzia meli (Entrance Channel and Turning Basin), pamoja na maandalizi ya ujenzi wa gati lenye urefu wa kilomita 1.32 kwa ajili ya

kuhudumia meli kubwa za kisasa aina ya Megamax zenye uwezo wa kubeba hadi TEUs 24,000, ambazo kwa sasa haziwezi kuhudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam.

**ii. Bandari Kavu ya Kwala**

Serikali kupitia Tanzania Ports Authority imewekeza kiasi cha TZS bilioni 83.25 katika utekelezaji wa Mradi wa Bandari Kavu ya Kwala, ambao ulianza rasmi kutoa huduma za kibandari mwishoni mwa Julai 2025 baada ya kukamilika kwa maandalizi muhimu ya kiutendaji na miundombinu.

Kwa sasa shughuli za uendeshaji na utoaji huduma zinaendelea kikamilifu, ambapo wadau wote muhimu wakiwemo taasisi za Serikali zinazohusika na masuala ya bandari, forodha, usafirishaji na ukaguzi wa mizigo tayari wameanza kutekeleza majukumu yao katika Bandari Kavu ya Kwala kwa ufanisi. Kuanzishwa kwa bandari hiyo kumesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano wa shehena katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na kupunguza foleni za malori ndani ya Jiji la Dar es Salaam, hali iliyochangia kuongeza ufanisi wa huduma za usafirishaji, biashara na mnyororo wa ugavi kwa ujumla.

Aidha, kutokana na maboresho makubwa yanayoendelea kufanyika katika Bandari ya Dar es Salaam, kiwango cha shehena kinachoingia na kutoka bandarini kimeendelea kuongezeka kwa kasi. Hali hiyo imeongeza umuhimu wa matumizi ya Bandari Kavu ya Kwala kama kituo muhimu cha kuhudumia, kuhifadhi na kurahisisha usafirishaji wa shehena kwa ufanisi zaidi, sambamba na kuimarisha ushindani wa sekta ya usafirishaji na biashara nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Kwa upande mwingine, Serikali kupitia Tanzania Ports Authority pia imetenga maeneo maalum kwa ajili ya nchi nane za Ushoroba wa Kati katika eneo la Bandari Kavu ya Kwala, kwa lengo la kuimarisha biashara ya kimataifa na huduma za usafirishaji wa mizigo katika ukanda huo. Hadi sasa, Serikali ya Burundi imeanza ujenzi wa uzio katika eneo ililotengewa, huku Democratic Republic of the Congo ikiwa tayari imepata mwekezaji na kukabidhiwa rasmi eneo kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu na uwekezaji husika. Kwa nchi nyingine zilizobaki, majadiliano ya kidiplomasia yanaendelea kupitia mifumo mbalimbali ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kuhakikisha zinakabidhiwa maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kiusafirishaji zitakazoongeza matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu ya Kwala.





*Bandari Kavu ya Kwala Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha*

## 2.5. SEKTA YA NISHATI

Shirika la umeme Tanzania Mkoa wa Pwani hadi kufikia mwezi Machi, 2026 linahudumia wateja wapatao 305,885. Malengo ya shirika kwa mwaka 2025/26 ni kuunganisha wateja 57,557. Hadi kufikia machi, 2026 wateja 32,513 wameunganishwa sawa na asilimia 56.48.

### 2.5.1. Mkoa umetekeleza maelekezo yaliyotamkwa kwenye ilani mahususi kwa Mkoa wa Pwani katika sekta hii kama ifuatavyo;

**Ibara ya 29; Kuimarisha Upatikanaji wa Nishati, Katika miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo: –**

**a) Kumalizia uunganishaji wa umeme kwenye vitongoji vyote vilivyobaki;**

Mradi huu unapeleka umeme katika vitongoji 15 kila jimbo ambapo kwa Mkoa wa Pwani ni vitongoji 135 na unagharimu TZS Bil 14.9 utanufaisha wananchi 4,142. Mkandarasi yupo site anaendelea na ujenzi na ameshawasha vitongoji 133 kati ya vitongoji 135 sawa na asilimia 98.5. Mradi huu unaelekea ukingoni na unategemea kukamilika Septemba 2026.

Miradi ya usambazaji umeme vijijini inayotekelezwa chini ya wakala wa nishati vijijini REA, Vitongoji vilivyonufaika na miradi hii ni kama ifuatavyo;

**i. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo**

Vitongoji 15 ambavyo ni Masogola, Makondeko, Bwembweni, Goba, Zombengalawa, Vihagata Shule, Mtakuja “A”, Mwanansenge, Mwavi “A/B”, Mchanga Kichwa “B”, Dagaza, Chaga “B”, Mnamata, Kwadosi na Aman.

**ii. Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze.**

Vitongoji 15 ambavyo ni Mazingara, Mpaji (Voda), Komkwazu, Mnazi Mmoja, Komkomba, kwedikanga E, Kudigongo, Changa, Mindu Bwawani, Friends Corna, Msigi (Mlamindu), Visakazi Mashariki, Pera(Kwa Wagogo), Bwilingu(Mipalala) na Kisakisari.

iii. **Manispaa ya Kibaha**

Vitongoji 15 ambavyo ni Miyomboni, Saeni, Check Point, Simbani, Vitendo, Saeni KKT, Mkomboz, Zegeleni, Bwawa Madabala, Vifusini, Bwawa Hekani, Lulanzi, Sagale Kambini na Mikongeni.

iv. **Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha**

Vitongoji 14 anbavyo ni Soga Kongo, Ngohinge, Milalazi, Mavua, Kuyu, Kiseka, Muyombo Ufugaji, Tkalas, Kigogo, Kibaoni, Mkarambati, Kwala, Msuwa, Makazi Mapya na Mpiji Station..

v. **Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti**

Vitongoji 15 ambavyo ni Nyamanjenga, Mkwandara, Mipirani, Milonzi, Kikimbili, Kingweti, Bani, Doka, Kiongoro, Malenda, Mtanga, Usimbe Kidogo, Kipoka, Mkole, Mkegeton, Njia Nne, Zogoali, Kichangini, Nyambalapi, Mkwende, Nyang'undu, Nyakiro, Mkundi, Dimani "A" na Zimbwini.

vi. **Halamshauri ya Kilaya ya Kisarawe**

Vitongoji 15 ambavyo ni Kwasi, Kwa Madogo, Chang'ombe, Sungura, Majumba Sita, Kurui A, Sungwi Kati, Mbebetini, Umoja, Kinyemvule, Visima Vitatu, Kwa Maleta, Mikungugu, Ndogoyo na Mwembehasara.

vii. **Halmashauri ya Wilaya ya Mafia**

Vitongoji 14 ambavyo ni Ng'okwe, Tongola, Ruma, Mlola, Manywaga, Simba, Umbwerani, Sikula, Kiluli, Mpafuni, Mikoman, Ng'ombeni, Kivuni na Kibisini.

viii. **Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga**

Vitongoji 15 ambavyo ni Kerekese, Mazmla, Mbopo, Kimbangulile "E", Uzizi Kitonga, Kitumbo, Rabika, Bukini, Beta, Kikumbo, Ngalambemba, Mbebetini, Msufini, Kisangarawe na Cheta.

ix. **Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji**

Vitongoji 15 ambavyo ni Mpima Kibinda, Mparange, Makarafati, Njogoro, Mparange, Mbwara Mashariki Msikitini, Kiegele, Kipoka Msomeni, Msikitini, Chumbi Magharibi, Kwampakwila, Londondo, Kiwili, Nyawanje/Ngwembele na Namakono.

Aida Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ameshaanza kutekeleza Mradi wa HEP 2B ambao ni mradi wa awamu ya pili inayotekelezwa kwenye vitongoji 330. Mradi huu unagharimu jumla ya TZS. 46,693,840,847.46 ambapo unatarajiwa kukamiliki mwezi Juni, 2026. Vitongoji vitakavyonufaika na mradi huu ni kama ifuatavyo;

i. **Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo**

Vitongoji 21 ambavyo ni Vihagate, Engelo, Mkwama, Mlatange, Lusako, Segwa, Kudihaba, Mtakuja “B”, Vigwaza, Kinyemvuli, Magharibi, Sengasenga, Kulwi, Mandawe, Baukani “B”, Kimeremeta, Changoi, Ukwamani, Chombe Juu, Kiegea “A” na Kajiungeni.

ii. **Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze**

Vitongoji 21 ambavyo ni Kunduchi, Wamakonde, Minazini, Njia Panda, Kingubwi, Pugini, Zunga, Ludiga, Mwana, Kibwengo, Umasaini, Kipera “B”, Kudihungo, Kwadibago, Mbuyu “A”, Mindu Mlimani, Kwedikwiji “A” na “B”, Tengeni, Mazimunyu, Chang’ombe, Mpaji Mungu, Komzinge, Takalagane, Kwangomero, Nadanya, Nung’ulu, Mwerungwi, Mabega “B”, Mtupeni, Kwamwala, Msinune “B”, Msaganguvu, Mifugoni, Mafungo, Tongoni, Kwamaraha, Kivu, Kilemela “B”, Msikitini, Kalimeni, Kwedikanga “C” na “E”, Mbuyuni, Mkwajuni, Salen Juu, Mbukwa, Minduliugata, Makole, Kisogo na Mbuyu “B”.

iii. **Hamashauri ya Wilaya ya Kibaha.**

Vitongoji 18 ambavyo ni Vinyenze, Waya, Kwa Dosa, Kwa Pazi, Umasaini, Madimla, Mtongani, Disunyara kwa Mafather, Gude, Mguluka, Mtonga “B”, Miyombo Ukulima,Masaki, Mizuguni “B”, Miswe Duka, Mkoleni, Ngohingo Saeni na Kigelo kwa Udugu.

iv. **Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti**

Vitongoji 53 ambavyo ni Ndechamula, Nyambangala, Pwani, Kumbacha, Mchinga, Azimio, Lugome, Kiwaga, Mbawa (AGO kwa Hussein), Zumbe, Unyamlani, Salale, King’ongo, Matimbwani, Mfisini “A”, Ulongoni, Twana, Nyafeda, Mungutwa, Uwandani, Mfisini “B”, Mbumi, Mkopi, Kisimbya, Uponda Chini, Usimbe Kiwanjani, Goloatanga, Beta, Halisi, Nyunguni, Mtomboloka, Nyamakingili, Mjengea, Mjimwema, Mpafuni, Kariakoo, Mkale, Kibwibwi, Kipenya, Gosa, Bonjo, Nyamakingili, Mjengea, Mjimwema, Mpafuni, Kariakoo, Mkale, Kibwibwi, Kipenya, Gosa, Bonjo, Mdai, Mkilika, Nyamanjenga, Mkwandara, Mipirani, Milonzi, Kikimbili, Kingweti, Bani, Doka, Kiongoro na Malenda.

v. **Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe**

Vitongoji 64 ambavyo ni Bwawani, Videte, Mwendapole, Kifuru Timtim, Mzambarauni, Mkenge, Bondeni, Mihugwe, Makutupola, Msese, Kijang’ande, Taliani, Mayasa, Chang’ombe, Pangani, Ngobwe, Jaribu Tena, Visima Vitatu, Kwa Ponza, Egeya, Muwada, Mbuguni, Sobondole, Kiseto, Viyombo, Kurui B, Shuleni, Mkoga, Mwelanzi, Mgama, Mtuna, Kwa Mbetela, Mtitu, Kwa Zavu, Kwa Goma, Sembe, Msegamo B, Mnanila, Gelelo, Msikitini, Mangungu, Tondo, Bangu, Kitonga Chini, Viwege, Kifuru, Lukose, Lubane, Kitamba, Manolo, Mikulugile, Majichumvi, Kibungo, Vikungu, Malagala,

Kitondwe B, Mhaga Shuleni, Mtwini, Sungwi Kaskazini, Sungwi Mashariki, Kibweni, Fukwi, Nzasa na Ngugu.

**vi. Halmashauri ya Wilaya ya Mafia**

Vitongoji 19 ambavyo ni Mlundo, Mikongoni, Mkamba, Vuleni, Mikomani, Kivuni, Ngwena, Kidele, Kiwawe, Mwawani, Kipandeni, Kisimani Mafia, Ng'ombeni, Purura, Changarama, Bungara, Unyambwa "A", Ukunda na Mkarangama.

**vii. Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.**

Vitongoji 74 ambavyo ni Nyandege, Vikeze, Mgola, Mitawa, Beta, Nyamla, Nyamikalango, Kembani, Nyasikinze/Kizimu, Kwajagwa, Kikonga, Ziweziwe, Rugeke, Mchikichini, Vikonge, Gogo, Kitoho, Nyamwage, Madimka, Pundi, Nyambwawa, Nyavinondo, Nyamikuta, Kinyembanyemba, Ndoleni, Nyangobo, Mitoboto, Mwasani, Mperani, Shimo la Udongo, Mtyeke, Kilimamkongo, Mzaya, Misasa, Kokobo, Mahingi, Mwanahanika, Lugwadu, Mashariki, Bingachana, Nyingome, Kinzae, Utunge "C", Nyakele, Vikangala, Chasimba, Kondo Mwelanzi, Kidete, Kofi "A", Ngarawani, Chungu, Ngunguluka, Msonga Kusini, Chakande, Bombwe, Msorokelo, Ndondwa, Magogo, Mduzi, Milende, Kingoma Magharibi, Kidugo, Mtunduma, Kipote, Kilembea, Kibupuni, Mikolekole, Kikurwi, Msonga Kaskazini, Kidala, Tambalale, Mbopo, Uzizi Kiziko, Kimanyile na Mzingezinge.

**viii. Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji**

Vitongoji 31 ambavyo ni Mji Mwema, Mitumba, Misimbo, Kipei, Kipoka, Nyautika, Kisangi, Kifulu, Mkwiri, Siasa, Kungulwe, Nyarwiru, Kipugira, Kitundu, Kiwili, Mbunju, Beta, Nyipara, Karakana, Kitapi Mashariki, Kitapi Magharibi, Mihangalaya, Kikobo, Ipengo, Msikitini, Chumbi Magharibi, Nyakipande, Londondo, Mihilu, Makenzi na Nyandote.





*Usambazaji Umeme katika Vijiji na Vitongoji*

b) **Kuwezesha matumizi ya nishati safi kwenye taasisi 540 za umma na kutoa elimu kwenye kaya 121,270;**

Kipindi cha Januari 2026 hadi Machi 2026, Wakala wa Nishati Vijijini na Mijijini (REA) imetoa elimu ya nishati safi kwa wananchi 121,035 kupitia mikutano ya vijiji na mitaa 34 na kusambaza majiko ya nishati safi 361 kwa wananchi na taasisi mbalimbali . Aidha, utekelezaji wa miradi ni kama ifuatavyo;-



*Matumizi ya Nishati safi Shule ya Sekondari Mwinyi Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*




*Mradi wa Usambazaji Gesi ya Kupikia katika Nyumba za Wananchi Kijiji cha Kisemvule, Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

i. **Upelekaji wa nishati jua katika vijiji vilivyopo visiwa vya Kwale, Koma, Kuruti, Bwejuu, Mfisini, Jaja, Pombwe, Ruma na Ngonyang**

Mradi huu unalenga kupeleka nishati jua kwa kila nyumba "stand alone solar system" wenye uwezo wa 50wp, 80wp na 100wp. Mradi huu una wakandarasi wawili ambao ni **M/S Green Leaf Technology Solution Company Limited** na **M/S Trinity Solar Energy Limited** kwa gharama ya mradi huu ni TZS. **1,371,265,944.00** ambapo serikali itagharamia TZS. **935,081,337.60** na kiasi kilichobaki kitagharamiwa na wananchi kulingana aina ukubwa anao hitaji**.** Kwa sasa wakandarasi wanaendelea na upimaji na uagizaji wa vifaa. Kwa mkoa wa Pwani.

**Jedwali Na. 3 Idadi ya Stand Alone Solar zitakazosambazwa katika Visiwa vya Mkoa wa Pwani**

| LOT | 50WP | 80WP | 100WP |
|---|---|---|---|
| 15 | 644 | 269 | 161 |
| 16 | 294 | 123 | 74 |
| 17 | 406 | 169 | 101 |

ii. **Mradi wa usambazaji wa mitungi ya gesi ya kg 6 awamu ya II**

Mradi huu unahusisha usambazaji wa mitungi ya gesi ya kilo sita (6) ipatayo **22,785** kupitia kampuni ya **Manjis Gas Limited** kwa wilaya saba za mkoa wa Pwani. Kila wilaya itapata idadi ya mitungi **3,255** ambayo inauzwa kwa bei ya ruzuku ya asilimia 50 sawa na **TZS 17,500.** Bei hiyo inajumuisha gharama ya mtungi ukiwa na gesi, kichomeo pamoja na figa. Gharama ya mradi huu kwa ni **TZS 398,737,500**. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 machi, 2026, jumla ya mitungi **16,275** imesambazwa sawa na asilimia 71.43 na usambazaji unaendelea.

**Jedwali Na. 4 : Hali ya Usambazaji wa Mitungi ya Gas kwa kila Wilaya ya Mkoa wa Pwani**

| NA | WILAYA | IDADI ILIYOPANGWA | IDADI YA MITUNGI ILIYOSAMBAZWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Bagamoyo | 3,255 | 3,255 | 100 |
| 2 | Kibaha | 3,255 | 3,255 | 100 |
| 3 | Kibiti | 3,255 | 0 | - |
| 4 | Kisarawe | 3,255 | 3,255 | 100 |
| 5 | Mafia | 3,255 | 0 | - |
| 6 | Mkuranga | 3,255 | 3,255 | 100 |
| 7 | Rufiji | 3,255 | 3,255 | 100 |
| | **JUMLA** | **22,785** | **16,275** | **71.43** |

**iii. Mradi wa usambazaji wa majiko banifu**

Mradi huu unahusisha usambazaji wa majiko banifu yanayotumia kuni na mkaa kidogo ili kupunguza matumizi ya vyanzo hivyo vya nishati pamoja na athari za moshi zitokanazo na matumizi katika majiko ya kawaida. Mikataba hii imesainiwa tarehe **9 Mei, 2025** na itatekelezwa ndani ya **miezi 15**. Gharama ya mradi ni **TZS 596,400,000.00** ambapo serikali itatoa ruzuku ya **TZS. 477,120,000.00**. Mtoa huduma ni **L'S SOLUTION LTD** ambapo jumla ya majiko banifu **12,425** yatauzwa kwa wananchi kwa bei ya ruzuku. Gharama ya jiko moja ni TZS 56,000 kabla ya ruzuku, hivyo serikali itatoa ruzuku ya asilimia 80 sawa na TZS 44,800 na mwananchi atanunua jiko hilo kwa **TZS. 11,200.**

Majiko haya yatasambazwa katika wilaya saba za Mkoa wa Pwani kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini.

**Jedwali Na. 5: Usambazaji wa Majiko Banifu kwa kila Wilaya ya Mkoa wa Pwani.**

| NA. | WILAYA | IDADI ILIYOPANGWA | GHARAMA YA MRADI (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Bagamoyo | 1,775 | **596,400,000.00** |
| 2 | Kibaha | 1,775 | |
| 3 | Kibiti | 1,775 | |
| 4 | Kisarawe | 1,775 | |
| 5 | Mafia | 1,775 | |
| 6 | Mkuranga | 1,775 | |
| 7 | Rufiji | 1,775 | |
| | **JUMLA** | **12,425** | |

**iv. Mradi wa usambazaji wa gesi asilia kwa ajili ya kupikia katika Wilaya ya Mkuranga.**

Mkataba wa Utoaji wa ruzuku kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia majumbani kwa wakazi ya Mkoa wa Pwani na Lindi ulisainiwa tarehe **21 Juni, 2024** kati ya Wakala wa Nishati Vijijini na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Gharama ya mradi huu ni **TZS. Bilioni 13,272,334,135.45** ambapo Wakala unatoa ruzuku ya **TZS. Bilioni 6,817,284,882.95** sawa na asilimia 51.4 ya gharama ili kuwezesha utekelezaji wake. Aidha gharama iliyobaki itagharamiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Mradi huu umehusisha usambazaji wa gesi asilia kwa urefu kilomita 21.5 kwa wateja 529. Mradi huu unatekelezwa katika wilaya ya Mkuranga.

v. **Ufungaji wa Mifumo ya LPG**

Mifumo ya LPG imefungwa na katika gereza la Utete, Mkuza, Kilombero na Mafia. Mifumo hiyo bado haijaanza kutumika kwa sababu bado Magereza wapo katika hatua ya manunuzi ya mtoa huduma wa kusambaza majiko yatakayotumia LPG.

vi. **Ujengaji wa miondombinu ya bayogesi**

Magereza wameshampata mtoa huduma wa kujenga miundombinu ya bayogesi ambaye ni CAMARTEC na sasa wapo katika hatua za manunuzi ya vifaa vitakavyotumika katika ujenzi wa miundombinu hiyo. Jumla ya magereza matatu ya Mkoa wa Pwani yatafungiwa miundombinu hiyo kama ifuatavyo;

**Jedwali Na. 6: Mchanganuo wa mifumo ya bayogesi itakayofungwa na kusambazwa**

| NA. | MAGEREZA | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Kigongoni | Mfumo 1 wa bayogesi na majiko banifu 3 |
| 2 | Ubena | Mfumo 1 wa bayogesi na majiko banifu 3 |
| 3 | Kibiti | Mfumo 1 wa bayogesi na majiko banifu 3 |

**Ibara ya 29: Katika kipindi cha miaka mitano ijayo ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2025 – 2030 itaielekeza Serikali Kuimarisha Upatikanaji wa Nishati, Kwa kutekeleza miradi ya maendeleo inayogusa sekta za miundombinu kwa lengo la kuinua maendeeleo ya Mkoa na ustawi wa Wananchi.**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme katika Mkoa wa Pwani. Miradi ya kimkakati inayofanyika Mkoa wa Pwani ambapo inalenga utengenezaji na uimarishaji wa miundombinu ya umeme kwa ajili ya kurahisisha na kuboresha upatikanaji wa huduma ya umeme kwenye maeneo mbalimbali. Miradi hii ya kimkakati inaendelea kufanyika na ipo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo;

i. **Upanuzi wa kituo cha kupozea umeme Mlandizi kutoka 120MVA hadi 240MVA – Mlandizi.**

TANESCO inaendelea kutekeleza Upanuzi wa kituo cha Mlandizi kutoka 120MVA hadi 240MVA chini ya mradi wa TTGRUP kwa gharama ya TZS. Bilioni 15. Mkandarasi ambaye ni TBEA anendelea na kazi. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 98% na unatarajiwa kukamilika tarehe 20 Juni, 2026.



*Kituo cha Kupoza Umeme Mlandizi Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha*

ii. **Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Zegereni 2x120MVA, Kibaha Manispaa**

Kiasi cha TZS. Bil 54.73. kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha MVA 240 kwa uwekaji wa Transfoma mbili (2) zenye uwezo wa MVA 120 kila moja ili kuendana na ongezeko la viwanda. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 5% ambapo upo katika hatua ya ulipaji fidia Wananchi. Mkandarasi aitwaye Xian Electric kutoka China yupo katika hatua ya usanifu wa kina katika eneo hilo.

iii. **Ujenzi wa Njia ya Umeme msongo wa 33kV (Submarine) Chole – Jibondo (8 km)**

Mradi wa TZS. Bilioni 9.35 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umeme kwa Visiwa(Vijiji) vya Juani na jibondo Wilaya ya Mafia. Mradi huu unahusisha kuweka waya unaopita chini ya bahari (Submarine Underground Cable). Mradi unatekelezwa na mkandarasi wa kizawa anayeitwa M/S Nakuroi Investment Company Limited. Wananchi wa Vijiji hivyo watanufaika na umeme huo, kazi inayoendelea ni usimamishaji nguzo na kuvuta waya kabla ya eneo ya maingilio ya bahari. Mradi umefikia 30%. Na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/27.

iv. **Ujenzi wa Njia ya Umeme msongo wa 33kV (Submarine) Kisiju – Mafia (70 km)**

Mradi huu bado upo hatua za awali.

v. **Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa 220kV Pugu–Dundani, km 58**

Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa 220kV kutoka Pugu hadi Dundani Mkuranga (Mkandarasi Steg International Services wa Tunisia) kwa gharama ya TZS. bilioni 49. Utekelezaji umefikia 13.24 %.

vi. **Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Dundani 2x120MVA**

Mradi huu unalenga kukabiliana na ongezeko la wateja wadogo pamoja na viwanda. Mradi unaendelea na upo katika hatua za awali kabisa ambapo mkandarasi anaendea na kazi ya Kusawazisha eneo la mradi(levelling). Utekelezaji umefika asilimia 11.98%.

vii. **Ujenzi wa Kituo kipya cha Msufini (Mkuranga) 400/220/33kV**

Mradi huu wa Kituo kipya cha Msufini unagharimu kiasi cha TZS. bilioni 132 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha MVA 300 kwa uwekaji wa Transfoma mbili (2) zenye uwezo wa MVA 150 kila moja Transorma 2 zenye uwezo wa 90MVA kila moja ili kuendana na ongezeko la viwanda. Utekelezaji upo katika hatua ya ulipaji fidia Wananchi. Mkandarasi aitwaye TBEA kutoka China yupo ameanza utekelezaji, umefikia 30.5%.

viii. **Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa 400kV Chalinze–Kinyerezi–Mkuranga, km 125**

Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya 400kV kutoka kituo cha kupoza umeme Chalinze kwenda Mkuranga kupitia Kinyerezi( 136km) na Mkandandarasi anaitwa M/s TBEA Co. ltd kutoka China . Gharama ya mradi ni TZS. bilioni 158.94 na kazi ya utekelezaji wa mradi huu inaendelea na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2026. Utekelezaji umefikia 66.66%.

ix. **Ujenzi wa Kituo cha Kutolea Njia za Umeme(Switching Station) Tumbi**

Ujenzi wa kituo hiki kilichopo Kibaha eneo la Tumbi unagharimu kiasi cha TZS. Bilioni 2.9. Kituo kitakuwa na uwezo wa kutoa laini tano ambazo zitahudumia maeneo ya TAMCO Viwandani, Pangani, Maili Moja, Kwa mathias, Soga na maeneo ya karibu. Mkandarasi aitwaye M/S EZEETEC Limited anaendelea na kazi, Mradi huu umeanza 01/08/2025 na unatarajia kukamilika 02/08/2026. Utekelezaji umefikia 70%.

x. **Ujenzi wa njia mbili za umeme wa msongo wa 33kV** kutoka kituo cha kupooza umeme mlandizi (250MVA, 132/33kV) yenye urefu wa 46.8kM kwa lengo la kuimarisha umeme (voltage improvement) katika maeneo ya Bagamoyo hasa mapinga, kerege na zinga. Mradi umetekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia shirika la umeme Tanzania na kukamilika tarehe 19 Aprili, 2026 kwa gharama ya TZS 3.177Billions.

## 2.6. SEKTA YA MAJI

**Ibara ya 37 ya Ilani ya CCM yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa Maji kwa Wananchi wote, Kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa Wananchi kutoka asilimia 85.15 hadi asilimia 95.56.**

### 2.6.1. Pamoja na kutekeleza Maelekezo Mahususi kwenye Serikali imetekeleza pia Maelekezo ya Jumla katika Sekta ya Maji Vijijini kama ifuatavyo:-

Mkoa una jumla ya vijiji 410 na mitaa 109, hadi sasa vijiji 394 vinapata huduma ya maji yenye kujitosheleza na vijiji 16 havina huduma ya maji. Hali ya upatikanaji maji ni sawa na asilimia 88.65 ya wakazi wote wa Mkoa, ikiwa asilimia 84.3 ya wakazi waishio Vijijini na asilimia 93 ya wananchi waishio mijini.

i. Katika kipindi cha kuanzia Machi, 2021 mpaka Machi, 2026 Serikali imetekeleza na kukamilisha jumla ya miradi 67 katika vijiji 78 kwenye Wilaya 7; Wilaya ya Mafia (Jojo,Bweni, Mibulani, Kidika, Chunguruma, Jibondo, Kifinge na Banja), Wilaya ya Rufiji (Tawi, Mtanza, Mohoro, Chumbi, Siasa, Nambunju, Mkongo na Nyamwage),Wilaya ya Kibaha (Minazimikinda, Mpiji, KimaraMisale, Kitomondo, RuvuStation, Kwala, Lukenge), Wilaya ya Kibiti (Jaribu Mpakani, Kikale, Mtunda, Kilulatambwe, Mchungu, Mahege, Kivinja "A", Mjawa, Miwaga, Ngulakula na Ruaruke), Wilaya ya Kisarawe (Msanga, Mianzi, Mafizi, Boga, Mengwa, Vinga'andi, Kului, Pangaramwingereza, Chole, Kwala na Bembeza), Wilaya ya Bagamoyo (Lwazi, Mataya, Mandawe, Mlingotini, Kwamduma, Mkoko, Fukayosi, Chamgoi, Mtambani, Chauru, Pingo, Kidogozero, Kitonga, Milo, Diozile, Kwamsanja, Kwavuli, Tambala, Matipwili, Kidomole na Kitame) na Wilaya ya Mkuranga (Mkerezange, Kigoda, Mwanambaya, Yavayava, Msorwa, Kolagwa, Kalole, Nasibugani, Kimanzichana Magharibi, Kimanzichana Kusini, Kimanzichana Kaskazini na Nganje) iliyogharimu jumla ya TZS. 44,108,561,878.84 na kunufaisha wakazi 330,098 sawa na asilimia 10.2 ya wakazi wa Mkoa. Aidha miradi 24 katika vijiji 68 yenye gharama ya TZS. 17,000,911,549.31 inaendelea kutekelezwa. Miradi 11 inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2026 na kunufaisha wakazi 38,955 (sawa na asilimia 1.9) hivyo kufikia asilimia 86.2 ya kiwango cha upatikanaji maji safi na salama kwa wakazi waishio vijijini;



*Mradi wa Maji katika Kijiji cha Ndundutawa Halmashauri ya Mji Rufiji*




*Mradi wa Maji katika Kijiji cha Sotele Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*




*Uzinduzi wa Mradi wa Maji katika Kijiji cha Sotele Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*




*Mradi wa Maji katika Kijiji cha Mlanzi Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti*

ii. Pia katika utekelezaji wa program ya uchimbaji wa visima 900, Mkoa umetumia jumla ya TZS. 3,299,154,740.81 kwa ajili ya kazi ya utafutaji wa vyanzo vya maji, uchimbaji visima na ujenzi wa vizimba katika maeneo 40 ya Mkoa. Jumla ya visima vya maji (34) vimekamilika,Maunganisho kutoka bwawa la mjembe (1) na maunganisho (5) kutoka bomba kuu la DAWASA yamekamilika.

**2.6.2. Serikali imetatua kero ya upatikanaji wa Maji kupitia Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) kama ifuatavyo: –**

**a) Kuongeza Upatikanaji wa Huduma ya Maji**

Kuongeza idadi ya wateja waliounganishiwa huduma ya maji kutoka kaya 33,236 hadi kufikia kaya 37,591 machi, 2026.

i. Kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kufikia wastani wa asilimia 93; na

ii. Kuendelea kuboresha mtandao wa maji katika kata zote 13 zinazohudumiwa.

**b) Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati**

i. Kuanzishwa kwa Mradi wa Maji Tamco – Pangani wenye thamani ya Tsh bilioni 8.99, unaolenga kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 20 hadi kufikia asilimia 95 katika maeneo ya Pangani na kata jirani; na

ii. Kuendelea na miradi ya usanifu na utekelezaji katika kata zenye changamoto ya maji kama;-

- **Kata ya Viziwaziwa**
  Tayari umefanyika usanifu wa mradi mkubwa wa maji ambao utamailiza kero ya maji eneo lote la Viziwaziwa na mitaa yake yote. Mradi utahusisha ujenzi wa mtandao wa bomba urefu wa km 38.191, ujenzi wa Tanki lenye ujazo wa lita Milioni 1 na laki tano na utagharimu kiasi cha TZS. bilioni 6.5 ambapo kwa sasa usanifu bado unaendelea.
- **Kata ya Kongowe**
  Usanifu umefanyika wa mradi mkubwa wa maji ambao utamaliza kero ya maji eneo la Kata ya Kongowe na mitaa yake yote. Mradi utahusisha ujenzi wa mtandao wa bomba urefu wa km 5.540 na huu utagharimu kiasi cha TZS. 177,332,099.25 millioni ambapo kwa sasa usanifu umeshakamilika kwa utekelezaji.
- **Kata ya Soga**
  Usanifu umefanyika wa mradi wa maji ambao utamaliza kero ya maji eneo la Kata ya Soga kitongoji cha Kigero. Mradi utahusisha ujenzi wa mtandao wa bomba urefu wa km 3.959 kwa upande wa kigero na huu utagharimu kiasi cha TZS. 81,564,474 na utekelezaji unaendelea.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA ILANI YA CCM KISEKTA KATIKA MAENEO MENGINE YENYE MAELEKEZO YA JUMLA

**Mkoa wa Pwani umeendelea na utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya CCM katika maeneo yenye Maelekezo ya Jumla katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo;-**

### 3.1. SEKTA YA VIWANDA

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 23(a) ya Ilani ya CCM; Kuandaa na kuhuisha wasifu wa uwekezaji wa mkoa na wilaya. Mkoa umefanikisha kufanya yafuatayo;-**

Kuandaa mwongozo wa uwekezaji ambao utaambatana na wasifu wa uwekezaji wa kila Wilaya na Mkoa kwa ujumla ambapo kazi imefikia asilimia 30 ya utekelezaji.

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 23(b) ya Ilani ya CCM; Kutenga maeneo ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta 101,798 katika maeneo ya Chamakweza, Razaba, Kwala, Ruvu, Magindu, Soga, Kikongo, Zegereni, Mbwawa Pangani, Misugusugu, Jaribu Mpakani, Bungu na Mtawanya, Visegese, Mbezi, Chemchemi Nyamato na Mkiu. Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

Mkoa kupitia Halmashauri zake zote tisa (9) umetenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji ambapo Kongani (Industrial and Agricultural Parks) na Maeneo Maalum ya Uwekezaji (Investment Zones) kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, Maeneo hayo yameongezeka kutoka 27 mwaka 2025 hadi 34 mwaka 2026, Maeneo haya yana jumla ya Ekari 116,718.39.

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 23(c) ya Ilani ya CCM; Kujenga miundombinu wezeshi ikiwemo barabara, umeme na maji katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji; Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

i. Kibaha DC - Barabara yenye urefu wa KM 20 ya kutoka Nzinga hadi Ruvu Stesheni imechongwa kuingia eneo la uwekezaji Sino Dar na kuwekwa makalavati matatu kwa gharama ya TZS. 55,000,000;

ii. Maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Kinyerezi (Dar) hadi Chalinze unaendelea; Upembuzi yakinifu, Usanifu wa awali wa kihandisi na tathmini ya athari za mazingira unaendelea.



*Matengenezo ya Barabara ya kuelekea Kongani ya Sino-Dar iliyopo Kwala-Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha*

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 23(d) ya Ilani ya CCM; Kujenga kongani za viwanda 48 katika maeneo ya Tazara, Chamakweza, Kwala Dutumi, Magindu, Kikongo na Soga, Pangani, Mbwawa, Zegereni na Misugusugu, Visegese, Nyamato na Mbezi, Nyamwage, Kibiti; Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

Kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji ambapo Kongani (Industrial and Agricultural Parks) na Maeneo; maalum ya Uwekezaji (Investment Zones) kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, Maeneo hayo yameongezeka kutoka 27 hadi 34 mwaka 2026, Maeneo haya yana jumla ya Ekari 116,358.37 kama inavyoonekana kwenye Jedwali namba 7.

**Jedwali Na. 7: Mchanganuo wa Maeneo ya Uwekezaji Mkoa wa Pwani**

| Na. | HALMASHAURI | JINA LA KONGANI | KATA | EKARI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkuranga | Dundani | Mkuranga | 17.77 |
| 2 | Mkuranga | Dundani | Mkuranga | 66.72 |
| 3 | Mkuranga | Vikindu | Vikindu | 59.31 |
| 4 | Mkuranga | Kisemvule | Vikindu | 22.73 |
| 5 | Mkuranga | Kisemvule | Vikindu | 17.57 |
| 6 | Mkuranga | Mwanambaya | Mipeko | 42.01 |
| 7 | Mkuranga | Mkiu | Nyamato | 12,355 |
| 8 | Mkuranga | Soap and Allied Compan Lited -Kazole | Vikindu Kazole | 1,236 |
| 9 | Mkuranga | Kilua Industrial Park | Kiparang`anda | 52 |

| Na. | HALMASHAURI | JINA LA KONGANI | KATA | EKARI |
|---|---|---|---|---|
| 10 | Chalinze | Pingo | Pingo | 78 |
| 11 | Chalinze | Chamakweza | Pera | 247.11 |
| 12 | Mafia | Shamba la Nduji-Baleni | Nduji | 30.3 |
| 13 | Mafia | Mwamizi Ndagoni | Ndagoni | 600 |
| 14 | Mafia | Utumaini Ndagoni | Ndagoni | 4040 |
| 15 | Bagamoyo | Kamal Industrial Estate | Kerege | 352 |
| 16 | Bagamoyo | TISEZA Bagamoyo | Zinga na Kiromo | 24155.29 |
| 17 | Bagamoyo | Kongani ya Vijana | zinga | 60 |
| 18 | Kisarawe | Kisarawe Industrial Park | Kazimzumbwi | 2471.05 |
| 19 | Kibaha DC | Modern Industrial Park | Kikongo | 1077 |
| 20 | Kibaha DC | Kwala Industrial Industrial Park | Kwala | 2500 |
| 21 | Kibaha DC | Soga | Soga | 950 |
| 22 | Kibaha DC | Kikongo | Kikongo | 4957.5 |
| 23 | Kibaha DC | Kwala | Kwala | 502 |
| 24 | Kibaha DC | Dutumi - Madege | Dutumi | 2463 |
| 25 | Kibaha DC | TISEZA - Kwala | Kwala | 24,216 |
| 26 | Kibaha DC | Sino Dar | Kwala | 625 |
| 27 | Kibaha DC | Elsewedy | Kikongo | 650 |
| 28 | Kibaha DC | Gaini | Kikongo | 205 |
| 29 | Kibaha MC | Zegereni | Visiga | 21,057.29 |
| 30 | Kibaha MC | TAMCO | Tangini | 496.68 |
| 31 | Kibaha MC | Miyomboni | Misugusugu | 84.02 |
| 32 | Kibaha MC | Vikawe - Pangani | Pangani | 1123.61 |
| 33 | Kibaha MC | Misugusugu | Misugusugu | 1111.3 |
| 34 | Kibaha MC | Mbwawa | Mbwawa | 8,797.11 |

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 23(e) ya Ilani ya CCM; Kuandaa na kutekeleza mpango wa ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Binafsi. Mkoa umefanikisha yafuatayo:-**

Serikali inashirikiana na Sekta Binafsi kupitia vikao mbalimbali vya pamoja vya wadau wa sekta Binafsi na Umma "Public Private Dialogue" vikao hivyo vimeimarisha Mashauriano na Ushirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi katika kuboresha mazingira ya Uwekezaji na kufanya biashara. Kwa mwaka wa fedha 2025/26 hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya vikao 3 na baraza la biashara la Mkoa 1 limefanyika.

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 28(a) ya Ilani ya CCM; Kuongeza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda kutoka hekta 68,227.10 hadi hekta 103,331; Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

Kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji ambapo Kongani (Industrial and Agricultural Parks) na Maeneo Maalum ya Uwekezaji (Investment Zones) kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, Maeneo hayo yameongezeka kutoka 27 mwaka 2025 hadi 34 mwaka 2026, Maeneo haya yana jumla ya Ekari 116,358.37 ikiwa ni moja ya fursa zinazovutia uwekezaji katika Mkoa wa Pwani. Maeneo haya yanajumuisha maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) 5 (Kwala, Bagamoyo, Vigor SEZ, Min Xin na Kamal); kongani za viwanda 15 (Kwala, Modern,TAMCO, Dundani, Elsewedy, Grei, Gain, Soap and Allied, Kilua, Misugusugu, Mkiu, Kongani ya Vijana, Sinodar na Kibaha Industrial Park) na maeneo mengine 14 katika Wilaya zote ndani ya Mkoa.

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 28(b) ya Ilani ya CCM; Kujenga miundombinu ya maji, umeme na barabara katika maeneo ya viwanda ili kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji. Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

Kuendelea kuweka miundombinu wezeshi ya Barabara, umeme, maji kwa kushirikiana na taasisi husika kama DAWASA, TANROADS, TARURA, TANESCO, RUWASA n.k ili kuvutia zaidi wawekezaji kama ifuatavyo;-

i. Katika kuimarisha hali ya umeme viwandani eneo la Kwala, Zegereni na Mlandizi, Shirika limeongeza Transformer kubwa eneo la Mlandizi ya ukubwa wa 50MVA;

ii. Kisarawe DC - barabara yenye urefu wa Km 11 imechongwa kutoka Ofisi ya Serikali za Mitaa kuelekea eneo la viwanda Visegese pamoja na barabara za ndani za eneo hilo kwa gharama ya TZS. 13,000,000;

iii. Mkuranga DC - Barabara yenye urefu wa KM 10 kutoka Kisarawe II hadi kazole park kwa ajili ya kurahisisha kufika eneo la Kazole industrial Park (SOAP and ALLIED), imeboreshwa kiwango cha changarawe na kutengeneza madaraja 2 onesha yenye gharama kiasi gani, kazi za kupeleka umeme inaendelea;

iv. Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Kinyerezi (Dar) hadi Chalinze unaendelea; Upembuzi yakinifu, Usanifu wa awali wa kihandisi na tathmini ya athari za mazingira unaendelea; na

v. Usambaji wa maji katika maeneo ya viwanda unaendela ili kuwa upatikanajiwa maji ya kutesheleza katika uzalishaji Viwandani.

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 28(d) ya Ilani ya CCM; Kuanzisha na kuendeleza kongani za viwanda 49 na Maeneo Maalumu 10 ya Kiuchumi (SEZs), pamoja na maeneo huru 15 ya biashara. Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

Mkoa umeanzisha maeneo mapya saba (7) ya uwekezaji yenye ukubwa wa ekari 15,676 na kufanya Mkoa kuwa na jumla ya maeneo 34 ya uwekezaji yenye ukubwa wa ekari 116,358.37.

**Jedwali Na. 8: Mchanganuo wa Maeneo Mapya ya Uwekezaji**

| Na | Halmashauri | Jina la Eneo la Kongani | Kata | Mmiliki | Ekari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mkuranga DC | Mkiu | Nyamato | Kusini Gateway Co Ltd | 12,335 |
| 2. | Mkuranga DC | Soap and Allied Company Limited -Kazole | Vikindu Kazole | Baohoon Company Ltd | 1,236 |
| 3. | Mkuranga DC | Kilua Industrial Park | Kiparang`anda | Kilua Industrial Park | 52 |
| 4. | Kibaha MC | Misugusugu | Misugusugu | Wananchi | 1,111.3 |
| 5. | Kibaha DC | Sino Dar | Kwala | Sino Dar Co. Ltd | 625 |
| 6. | Kibaha DC | Gaini | Kikongo | Gaini | 205 |
| 7. | Bagamoyo DC | Kongani ya Vijana | Zinga | TISEZA | 60 |

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 28(e) ya Ilani ya CCM; Kuanzisha viwanda vikubwa 45, viwanda vya kati 71 na viwanda vidogo 182. Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

i. Kuongeza Idadi ya Viwanda kutoka Viwanda 1,631 hadi 1,722 Machi, 2026 Viwanda 226 ni vikubwa, 231 vya kati, 248 vidogo na 1,017 vidogo sana. Katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita jumla ya viwanda 335 vimejengwa kati ya viwanda hivyo 148 ni vikubwa, 121 viwanda vya kati, 66 viwanda vidogo kati ya hivyo, viwanda 82 vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

ii. Kuongeza ajira za moja kwa moja kutoka 20,112 mwaka 2025 hadi 22,289 mwaka 2026 na ajira zisizo za moja kwa moja zaidi ya 62,000.



*Kiwanda cha kuzalisha Vioo cha Keda (Keda Glass) kilichopo kijiji cha Mbezi Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 28(f) ya Ilani ya CCM; Kujenga mitaa 15 ya viwanda ambayo ina miundombinu muhimu kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo na vya kati. Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

Mkoa umetenga eneo jipya moja (1) kwa ajili ya kujenga mtaa wa viwanda lenye ukubwa wa ekari 60 ( Kongani ya Vijana). Eneo hilo lipo katika Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo. Taratibu za kuendeleza eneo hilo zinaendelea.

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 28(g) ya Ilani ya CCM; Kuongeza utoaji wa leseni za biashara kutoka 27,340 hadi 49,927. Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

i. Utoaji wa leseni za Biashara kutoka 27,340 kwa mwaka 2025 hadi 36,699 mwaka 2026;

ii. Kutoa elimu kuhusu biashara, Nembo ya Taifa ya Bidhaa, Ubora wa Bidhaa, Haki ya Mlaji kwa wafanyabiashara na wajasiriamali ambapo Jumla ya wadau 7,491 wamepatiwa elimu ya ujasiriamali; na

iii. Utoaji wa huduma za biashara na uwekezaji zimeboreshwa kupitia kituo cha huduma za pamoja “One Stop Center” kilichopo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani ambapo Taasisi Wezeshi 21 huwepo siku za Jumanne na Alhamisi ya kila Wiki ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa pamoja kukagua na kutoa ushauri wa kitaalamu. Aidha, huduma hutolewa katika ngazi za Halmashauri kupitia Madawati maalum ya Uwekezaji.

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 28(h) ya Ilani ya CCM; Kuongeza maeneo ya biashara kwa wafanyabiashara wadogo kutoka 521 hadi 1,554. Mkoa umefanikiwa kufanya yafuatayo;-**

i. Serikali imetenga maeneo maalum (masoko) kwa ajili ya Wafanyabiashara Wadogo (Wamachinga) katika Halmashauri zote. Mkoa unajumla ya masoko 43 ambayo yanatumiwa na wafanyabiashara.

ii. Mkoa una ofisi kwa ajili ya shughuli za Machinga katika Halmashauri ya Kibaha Mji iliyojengwa kwa fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri wa Tanzania.

## 3.2. SEKTA YA TEHAMA

**Kukuza na kuimarisha matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za kiuchumina kijamii.**

**Ibara 38 (d): Kuongeza maeneo ya umma yenye huduma ya mawasiliano ya intaneti yenye kasi ili kukuza matumizi sayansi na teknolojia;-**

Mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano katika Mkoa wa Pwani kupitia ujenzi wa kilomita 344 za Mkongo wa Taifa kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma bora za intaneti na mawasiliano ya uhakika kwa wananchi, taasisi na sekta mbalimbali za uzalishaji. Ujenzi huo umeiwezesha Serikali kuimarisha mazingira ya kidijitali na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi ndani ya Mkoa.

Aidha, Kituo cha Mkongo wa Taifa kimejengwa Wilaya ya Kibiti ili kuongeza upatikanaji na ubora wa huduma za mawasiliano kwa wananchi, taasisi pamoja na shughuli za viwanda katika maeneo jirani. Vilevile, huduma za mawasiliano katika eneo la Muhoro zimeboreshwa kwa kuunganishwa na Mkongo wa Taifa kupitia ujenzi wa kilomita 45 za miundombinu ya mawasiliano. Sambamba na hatua hiyo, ujenzi wa miundombinu ya kupeleka huduma za Mkongo wa Taifa katika eneo la Zegereni Industrial Park umeanza kwa urefu wa kilomita 22 kwa lengo la kuimarisha mazingira ya uwekezaji na maendeleo ya viwanda kupitia huduma za kisasa za mawasiliano.

Katika kuendelea kusogeza huduma za mawasiliano karibu na wananchi, Serikali imeimarisha huduma za Fiber ambapo wananchi 5195 wamefikiwa na huduma ya Fiber to the Home (FTTH). Huduma hii inawezesha wananchi kuunganishiwa intaneti ya kasi moja kwa moja majumbani na hivyo kurahisisha matumizi ya huduma mbalimbali za kidijitali ikiwemo biashara mtandao, elimu, mikutano ya mtandao, huduma za kifedha pamoja na upatikanaji wa taarifa kwa haraka na uhakika. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025/2030 inayolenga kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kuongeza upatikanaji wa huduma bora za mawasiliano kwa wananchi.

Katika kuendelea kusogeza huduma za mawasiliano karibu na wananchi, Katika mwaka 2025, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imeendelea kuboresha huduma za mawasiliano katika Mkoa wa Pwani ambapo jumla ya minara 30 ya mawasiliano imejengwa na kuwashwa katika wilaya mbalimbali za mkoa huo. Kati ya minara hiyo, Wilaya ya Bagamoyo imepata mnara 1, Kibaha minara 4, Kibiti minara 8, Kisarawe minara 8, Mafia minara 3, Mkuranga minara 5, na Rufiji mnara 1. Utekelezaji wa miradi hiyo umechangia kwa kiasi kikubwa kupanua huduma za mawasiliano hususan katika maeneo ya vijijini na maeneo yaliyokuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma za simu na intaneti.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026, UCSAF inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mawasiliano ya simu ambapo Mkoa wa Pwani umenufaika na jumla ya minara 17 mipya. Kati ya hiyo, minara 4 itajengwa kupitia mradi wa awamu ya 10 na minara 13 kupitia mradi wa awamu ya 11. Serikali kupitia UCSAF inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora za mawasiliano kwa lengo la kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kupitia juhudi hizi, wananchi wengi hasa wa maeneo ya vijijini wameendelea kunufaika na huduma za mawasiliano ambazo zimeimarisha shughuli za biashara, elimu, afya pamoja na upatikanaji wa taarifa muhimu kwa maendeleo ya taifa.

## 3.3. SEKTA YA ELIMU

**Katika utekelezaji wa Ibara ya 35 ya Ilani ya CCM**

Sekta ya Elimu imeendelea kufanya vizuri kwa kuhakikisha kuwa Wanafunzi wote wanapata fursa ya Elimu ya Msingi. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;-

**i. Serikali kuendelea kutekeleza Mpango wa Elimu bila Ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita;-**

Serikali imeendelea kutoa fedha kila mwezi kugharamia Elimu msingi bila malipo katika maeneo ya ruzuku ya uendeshaji wa shule (capitation), chakula, fidia ya ada ya wanafunzi na posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Maafisaelimu Kata. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Mkoa umepokea TZS. 15,757,952,914.00 kwa ajili ya shule za awali na msingi na Sekondari ambapo kati ya hizo Kiasi cha TZS. 4,399,941,947.00 ni kwa ajili ya elimu ya awali na msingi na kiasi cha TZS. 11,358,010,967.00 kwa ajili ya kugharamia Elimu ya sekondari.

**ii. Kuongeza idadi ya Shule za Msingi na Shule za Sekondari**

Fursa ya upatikanaji wa elimu ya Msingi na sekondari katika Mkoa imeogezeka kutokana na kuongezeka kwa idadi ya shule za Msingi kutoka 693 hadi 862 Machi, 2026 ambapo 662 ni za Serikali na 200 ni zisizo za Serikali na shule za sekondari kutoka 194 hadi kufikia shule 296 Machi, 2026 ambapo 197 ni za Serikali na 99 ni zisizo za Serikali. Ongezeko la

shule kutoka Julai 2025 mpaka Machi, 2026 ni shule 36. Ongezeko la shule za msingi ni 27 za serikali ni 12 na binafsi ni 15 na Sekondari ni 9 za Serikali ni 7 na Binafsi 2.



*Shule mpya ya Sekondari Mbezi Gongoni, Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

iii. **Kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa ya shule za msingi na madarasa ya shule za Sekondari.**

Mkoa umeendelea na juhudi za kuhakikisha unaongeza vyumba vya madarasa ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Hadi kufikia Juni, 2025 idadi ya vyumba vya madarasa vilikuwa 10,622 (Msingi 6,076, sekondari 4,546). Kutoka Julai, 2025 hadi Machi, 2026 vyumba vya madarasa vilivyojengwa ni 570 (msingi 312, sekondari 258) na kufanya jumla ya vyumba vya madarasa kufikia 11,171 (Msingi 6371, Sek 4800).



*Ujenzi wa madarasa mapya katika Halmashauri ya Mji Bagamoyo*

iv. **Kuongeza nyumba za walimu wa shule za msingi na sekondari.**

Mkoa umeendelea na juhudi za kuhakikisha unaboresha mazingira ya walimu kwa kuboresha makazi ikihusisha ujenzi wa nyumba za walimu. Hadi kufikia Juni, 2025 Mkoa ulikua na jumla ya nyumba za walimu 4,163 (Msingi 3,064, Sekondari 1,099). Aidha, Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya nyumba 52 (msingi 32, Sekondari 20) zimejengwa na kufanya jumla ya nyumba za walimu kufikia 3110 zikiwamo (Msingi 1696, sek 1414).

v. **Kuandaa na kutekeleza mpango wa kuwapatia chakula wanafunzi shuleni.**

Mkoa unaendelea kutekeleza mpango wa utoaji wa huduma ya chakula shuleni ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapata chakula wakiwa shuleni. Jumla ya wanafunzi ni 608,289 (msingi 441,981, sek 166,308) kati yao wanafunzi 402,802 (msingi 316,899 sawa na asilimia 71.70 na Sek 85,903 sawa na asilimia 51.65) wanapata chakula wakiwa shuleni. Juhudi za kuhakikisha wanafunzi wote wanapata chakula wakiwa shuleni zinafanyika.

vi. **Kujenga vyuo 6 vya ufundi (VETA)**

Mkoa katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025 umepokea fedha jumla sh. **13,104,514,004.97** kwa ajili ya ujenzi wa vyuo sita (6) kati ya 2 vimekamilika na vinatumika vya ufundi Stadi (VETA) katika Halmashauri za Wilaya za Mafia, Rufiji, Kibiti, Mkuranga, Chalinze na Kisarawe. Ujenzi wa vyuo hivyo vya VETA umekamilika na vinatumika.

vii. **Kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa darasa la saba kutoka asilimia 83 hadi asilimia 100, kidato cha nne kutoka asilimia 83 hadi 100 na kidato cha sita kutoka asilimia 98 hadi 100.**

Kiwango cha Ufaulu wa Mitihani ya Darasa la Saba umeongezeka kutoka asilimia 83.16 mwaka 2022 hadi asilimia 87.21 mwaka 2025, Darasa la Nne kutoka asilimia 88.14 ya mwaka 2022 hadi kufikia 89.12 ya mwaka 2025, Kidato cha Pili Kutoka asilimia 79.93 mwaka 2022 hadi asilimia 85.86 ya mwaka 2025, Kidato cha nne kutoka asilimia 83.84 mwaka 2022 hadi asilimia 93.60 mwaka 2025 na kidato cha sita ufaulu ni asilimia 99.85 kwa mwaka 2024 na kwa mwaka 2025 ni asilimia 99.59.

Ili kuhakikisha ubora wa elimu unaimarika na kuboresha ufaulu, Mkoa umeanzisha Matumizi ya Tehama katika Ufundishaji na Ujifunzaji. Hii itasaidia kutatua changamoto ya upungufu wa walimu hususan wa masomo ya sayansi na Hisabati. Shule 22 za Sekondari za Mkoa wa Pwani zimepatiwa vifaa vya TEHEMA kwa ajili ya uanzishwaji wa darasa janja. Shule hizo ni Bagamoyo Sekondari na Chasimba (Bagamoyo), Mbwewe (Chalinze DC), Kilangalanga, Ruvu, Samia Mtongani(Kibaha dc), Shimbo Mkuza, Kibaha Boys (Kibaha MC), Dr Samia Lumyozi, Kibiti (Kibiti DC), Jokate Mwegelo, Minaki, Kitanga Kisarawe (Kisarawe Dc), Raptha, Kidawendui

(Mafia DC), Kilimahewa, Kizapala, Kazole (Mkuranga), Bibi Titi Mohamed, Chemchem Rufiji, Rufiji, Ikwiriri (Rufiji TC). Halmashauri ya Manispaa ya Kibaha imetenga milioni 59 katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa ajili ya uanzishwaji wa darasa janja katika shule ya Sekondari Bundikani.

viii. **Kuongeza uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali** kutoka wanafunzi 158,538 hadi wanafunzi 205,736 darasa la kwanza kutoka 61,442 hadi 73,814, kidato cha kwanza kutoka 36,218 hadi 61,198 na kidato cha tano kutoka 7124 hadi 13,822.

a. **Uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali.**

Kwa mwaka 2026 Malengo ya uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali ni 57,655. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya wanafunzi wa awali walioandikishwa ni 42,638 sawa na asilimia 73.95.

b. **Uandikishaji wa Wanafunzi wa Darasa la Kwanza.**

Kwa mwaka 2026 Malengo ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza ni 57,689. Hadi kufikia tarehe 27.03.2026 jumla ya wanafunzi wa darasa la kwanza la kwanza walioandikishwa ni 60,626 sawa na asilimia 105.09.

c. **Uandikishaji wa Wanafunzi wa MEMKWA**

Kufikia tarehe 27.03.2026 wanafunzi wa MEMKWA walioripoti ni 477.

d. **Uripoti wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza**

Hadi kufikia machi, 2026 jumla ya Wanafunzi 34,102 wameripoti wakiwamo wavulana 15,666 na wasichana 18,436 sawa na asilimia 89.14 ya wanafunzi 39,590 waliochaguliwa.

ix. Mwaka 2025/2026 Mkoa umepokea TZS **7,873,124,370.40** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule za msingi na sekondari. Katika kiasi hicho TZS. **4,582,695,937.40** ni mapato ya ndani, TZS **1,756,265,925.00** zimepokelewa kutoka Serikali Kuu na TZS. **1,534,162,508.00** zimepokelewa kupitia Wadau mbalimbali, Wafadhili na Nguvu za Wananchi. Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **219**, matundu ya vyoo **252**, nyumba za walimu **18**, mabweni **15** na vyumba vya maabara **27**.

x. Mkoa umeimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwajengea uwezo Maafisa Elimu Kata 133, Walimu Wakuu 609 na walimu 4,181 kuhusu mbinu za kufundishia na kujifunzia. Pia Mkoa umewajengea uwezo katika ufundishaji na ujifunzaji walimu wa Elimu ya Awali 313 kuhusu matumizi ya njia shirikishi na vifaa vya Elimu ya Awali vilivyoboreshwa.

xi. Mkoa kwa kushirikiana na Shirika la Cambridge Education kupitia mradi wa Shule Bora umeanzisha zana ya utambuzi wa mabadiliko ya hali ya hewa utakaokuwa na uwezo wa kutambua mabadiliko ya hali ya hewa ili kuzuia majanga shuleni yanayoweza kusababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Zana hiyo inategemewa kukabidhiwa rasmi mwezi Machi 2026.

**xii.** Matumizi ya Tehama katika Ufundishaji na Ujifunzaji. Katika jitihada za kutatua changamoto ya upungufu wa walimu hususan wa masomo ya sayansi na Hisabati katika Shule za Sekondari Mkoa umeteua Shule ya Sekondari Kibaha kuwa kiungo cha Shule za Sekondari katika ufundishaji mubashara (Live Teaching) kwa kuwa vifaa vya ufundishaji vimefungwa katika madarasa mawili kwenye shule hiyo. Majaribio ya ufundishaji yamefanyika ambapo mwalimu wa shule ya Sekondari Kibaha ameweza kufundisha wanafunzi wa shule hiyo pamoja na wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Dodoma.

Mafanikio yaliyopatikana kupitia ufundishaji wa darasa janja yamesababisha kuwepo kwa haja ya kuongeza madarasa hayo nchini ambapo Serikali ilitoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchagua Shule ya Sekondari 1 (kila Halmashauri) na kutenga fedha kiasi cha TZS. 59,550,000.00 katika bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya miundombinu ya darasa janja moja au zaidi katika Shule zilizochaguliwa.

Ufundishaji wa darasa janja utasaidia kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu hususan katika masomo ya Hisabati na Sayansi, kukatisha masomo kutokana na kufungwa shule kunakosababishwa na mlipuko wa magonjwa na majanga mengine.

## 3.4. SEKTA YA AFYA

Mkoa una Jumla ya vituo vya kutolea Huduma za afya 635 kati ya hivyo 14 ni Hospitali, 61 ni Vituo vya Afya, na 440 ni Zahanati, 18 ni Kliniki, 6 ni "Maternity home" na 96 ni Maabara zinazojitegemea (Autonomous Laboratory). Hali ya umiliki; Vituo 373 vinamilikiwa na Serikali, 17 taasisi za umma, 41 Mashirika ya Dini na 204 binafsi.

**Ilbara ya 36(a)–(h); Kuendelea Kuimarisha Huduma bora za Afya; CCM itaisimamia Serikali Kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughulli za ujenzi wa Taifa na kuboresha maisha yao. Mafanikio yaliyopatikana hadi Machi 2026 ni kama yafuatayo:-**

a. Mwaka wa fedha 2025/2026 hadi kufikia Februari, 2026 Mkoa kupitia Halmashauri zake umepokea jumla ya TZS. 8,559,991,422 ambapo TZS. 2,742,370,000 ni kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa miundombinu katika hospitali za Wilaya, TZS. 3,532,185,478 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu kwenye vituo vya afya na TZS. 2,285,435,944 ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa zahanati.

b. Kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vifaa saidizi na vitendanishi kutoka asilimia 88.5 Oktoba - Desemba 2025 hadi asilimia 92 Januari - Machi, 2026. Pia mwezi Februari, 2026 yamefanyika mafunzo kwa timu za Halmashauri (Kibaha MC na Kisarawe DC) juu ya ufuatiliaji wa uwepo wa bidhaa za afya kituoni na kuweka mikakati ya kuondoa

ukosekanaji wa bidhaa hizo hivyo ni mategemeo uwepo wa bidhaa utaongezeka katika vipindi vya robo vijavyo.

c. Ili kuhakikisha huduma za dharura zinatolewa kituoni kwa makundi mbalimbali ya wagonjwa wakiwemo wale waliomahututi, majengo ya huduma za dharura sita yamejengwa katika Halmashauri ya Mafia, Rufiji, Bagamoyo, Chalinze, Kibiti, Kisarawe na Kibaha MC (hili lipo katika hospitali ya rufaa ya Mkoa-Tumbi). Pia kuna Majengo mawili ya wagonjwa mahututi katika Halmashauri ya Mafia na Kibaha MC (hospitali ya rufaa ya Mkoa - Tumbi).

d. Ili kufikisha huduma karibu na wananchi, kuna ongezeko la vituo vya afya vitatu (3) na kufanya idadi kufikia 61 na zahanati mpya saba (7) hivyo kufanya idadi ya zahanati kufikia 440. Aidha, maboma sita (6) ya vituo vya afya na maboma 16 ya zahanati yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kwa sasa asilimia 78.3 ya wakazi wa Mkoa wa Pwani wanasafiri umbali usiozidi kilomita tano (5) kufikia vituo vya kutolea huduma za afya.

e. Katika kuhakikisha huduma zinatolewa saa 24 vituoni, jumla ya nyumba za za watumishi 10 hivyo kufanya jumla ya nyumba za watumishi kuwa 381 sawa na asilimia 61 ya malengo yaliyowekwa kwenye Ilani ya mwaka 2025 - 2030 ya ujenzi wa nyumba za watumishi 624 za watumishi wa Afya.

f. Katika kutekeleza programu ya Bima ya Afya kwa Wote na kuongeza idadi ya Wananchi watakaofikiwa na huduma hiyo, Mkoa uameanza utekelezaji wa awamu ya kwanza wa sheria ya Bima ya Afya kwa Wote namba 13 ya mwaka 2023 kwa kutambua na kuwasajili kundi maalum la kaya za wananchi wasiokuwa na uwezo, ambapo jumla ya kaya 6,251 zenye wanufaika 25,680 zimetambuliwa. Kati ya kaya hizo, kaya 3,288 zimesajiliwa sawa na asilimia 52.6 ya lengo la usajili.

**Jedwali Na. 9: Mchanganuo wa Kaya Zilizotambuliwa na Kusajiliwa kwa ajili ya Bima ya Afya kwa Wote.**

| Na. | Halmashauri | Lengo (Kaya) | Zilizosajiriwa (Kaya) | Asilimia (Kaya) | Lengo (Wanufaika) | Waliosajiriwa (Wanufaika) | Asilimia (Wanufaika) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Bagamoyo DC | 225 | 144 | 64 | 927 | 380 | 41 |
| 2 | Chalinze DC | 997 | 200 | 20.1 | 4154 | 438 | 10.5 |
| 3 | Kibaha DC | 193 | 108 | 56 | 814 | 259 | 31.8 |
| 4 | Kibaha MC | 342 | 170 | 49.7 | 1535 | 414 | 27 |
| 5 | Kibiti DC | 1162 | 673 | 57.9 | 3991 | 1533 | 38.4 |
| 6 | Kisarawe DC | 628 | 364 | 58 | 2442 | 856 | 35.1 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Mafia DC | 54 | 33 | 61.1 | 217 | 60 | 27.7 |
| 8 | Mkuranga DC | 1436 | 788 | 54.9 | 6256 | 1993 | 31.9 |
| 9 | Rufiji TC | 1214 | 808 | 66.6 | 5344 | 2287 | 42.8 |
| | **Jumla** | **6,251** | **3,288** | **52.6** | **25,680** | **8,220** | **32** |

g. Katika kudhibiti na kumaliza vifo vitokanavyo na uzazi mkoa umeweza kupunguza vifo kutoka 51 kwa kila vizazi 100,000 mwaka 2024 hadi vifo 42 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2025, ambapo lengo la Kitaifa ni kufikia vifo 70 kwa kila vizazi hai 100,000. Mambo yafuatayo yamefanyika Hadi kufikia Machi 2026, mambo yafuatayo yamefanyika katika kufikia mafanikio haya:

   i. Ununuzi wa vifaa tiba vya kutosha na vyenye ubora;

   ii. Mafunzo elekezi kwa watoa huduma za afya ya uzazi ambapo katika kipindi cha Oktoba – Desemba, 2026 jumla ya watoa huduma 202 walipewa mafunzo;

   iii. Kuendesha vikao vya kujadili vifo vitokanavyo na uzazi lengo likiwa ni kutathmini sababu zilizochangia vifo vya akina mama na watoto vitokanavyo na uzazi vilivyotokea;

   iv. Kuboresha mifumo ya rufaa kwa wajawazito, wazazi na watoto wachanga kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma ya usafiri (ambullance za vituoni na madereva ngazi ya jamii kupitia mfumo wa M-MaMa;

   v. Kuongeza uwajibikaji katika ngazi zote ikilenga kuweka mipango kazi yenye mikakati ya kupunguza vifo na kuongeza ufuatiliaji; na

   vi. Kuongeza uhamasishaji kwa jamii juu ya kuanza kliniki ya ujauzito mapema na umuhimu wa kujifunguliakatika kituo cha kutolea huduma za afya.

h. Katika kupunguza udumavu kwa watoto wa chini ya miaka mitano na kuongeza huduma za lishe kwa makundi yanayoathirika zaidi ikiwa ni pamoja na wajawazito na vijana balehe, Mambo yafuatazo yamefanyika:-

   i. Halmashauri zimeendelea kutoa na kutumia fedha za Lishe zilizotengwa kwa Robo ya Januari hadi Machi, 2026 kwa asilimia 69.6;

   ii. Elimu ya Lishe imeendelea kutolewa katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya na ngazi ya jamii kwa asilimia 100;

   iii. Dawa za kuongeza wingi wa damu kwa wajawazito zimetolewa kwa wajawazito wote wanaohudhuria kliniki kwa asilimia 98.9; na

   iv. Nyongeza ya matone ya Vitamini A imetolewa kwa watoto chini ya miaka 5 katika Halmashauri zote kwa asilimia 100. Matone ya Vitamini A hutolewa kwa watoto chini ya miaka mitano mara mbili (2) kwa

mwaka kwenye kampeni ya mwezi wa Afya na lishe pamoja na kila siku za kliniki za watoto kwenye vituo vya huduma za Afya.

**Ibara ya 38; Katika kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na kuimarisha familia na ustawi wa makundi maalum, hadi kufikia Machi, 2026 Serikali ya Mkoa imetekeleza yafuatayo:-**

a. Kutekeleza mikakati ya kudhibiti ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto, wasichana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu. Jumla ya manusura 2477 (wanawake 2065 na wanaume 412) na mashauri 2728 ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto walipokelewa na kuhudumiwa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma kipindi cha Januari hadi Machi 2026. Hali hii imechangiwa na kuboreshwa kwa mfumo wa utoaji wa taarifa na uelewa wa jamii juu ya kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia. Aidha uwepo wa kamati za ulinzi wa Mwanamke na Mtoto ngazi zote pamoja na Wahudumu wa afya ngazi ya jamii ambao hushiriki kutoa elimu juu ya madhara ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya Watoto katika jamii;

b. Pia kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto pamoja na kuhakikisha mifumo ya malezi inazingatia uwajibikaji na utunzaji wa familia katika jamii. Kwa kushirikiana na shirika la BRAC Maendeleo vituo vya kijamii vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto vipatavyo saba vimeanzishwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Kibaha kufikia Machi 2026. Aidha Halmashauri inaendelea kusimamia utoaji wa huduma katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana vipatavyo 808 vilivyopo katika Halmashauri zote tisa (9) za Mkoa; na

c. Licha ya mambo hayo hapo juu pia kuna kuimarisha huduma za ustawi kwa wazee ikiwemo afya, matunzo, na ushirikishwaji katika maamuzi na shughuli mbalimbali za maendeleo. Hadi Machi, 2026 jumla ya wazee 71,141 wametambuliwa kati ya hao 42,693 (60%) wamenufaika na vitambulisho vya matibabu. Mabaraza ya wazee 523 yameundwa na kati ya hayo 403 yapo hai. Vyumba vya matibabu kwa wazee vimetengwa katika Hospitali zote tisa, aidha katika vituo vya afya na zahanati wazee na makundi mengine ya wasiojiweza hupewa vipaumbele wanapofika kupata huduma za afya.

**Ibara ya 36 (b) - (e): Katika kipindi cha miaka mitano ijayo ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 – 2030, CCM itaielekeza Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo inayogusa sekta ya Afya kwa lengo la kuinua maendeeleo ya Mkoa na Ustawi wa wananchi.**

Baadhi ya miradi hiyo katika sekta ya afya tayari imeshaanza kutekelezwa na baadhi ipo kwenye hatua za maandalizi, kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini, hali ilivyo ya utekelezaji Januari - Machi 2026.

| NA. | JINA LA MRADI | SEKTA | WILAYA/ HALMASHAURI | HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI JANUARI – MACHI 2026 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa majengo 2 ya wagonjwa wa nje (OPD) na RCH katika Vituo vya Afya Kerege na Fukayosi | Afya | Bagamoyo DC | o Ujenzi wa Jengo la OPD Katika kituo cha Afya Fukayosi umekamilika kwa 100% na linatumika.<br>o Ujenzi wa OPD kwa Kituo cha Afya Kerege badohaujatekelezwa na majengo ya RCH kwa vituo vyote hayajaanza kujengwa |
| 2 | Umaliziaji wa Zahanati ya Kitopeni (Kataya Kiromo) | Afya | Bagamoyo DC | Ujenzi umeanza kutekelezwa na umefikia hatua yakupaua sawa na 63% |
| 3 | Ujenzi wa Nyumba 65 za Watumishi Sekta ya Afya katika Hospitali ya Wilaya (11), Kituo cha Afya Miono (7), Kituo cha Afya Chalinze (4), Kituo cha Afya Msata (1), Kituo cha Afya Kibindu (3), Kituo cha Afya Lugoba (1), Kituo cha Afya Kwaruhombo (4), pamoja na Zahanati za Vijiji vya Vigwaza(2), Kiwangwa (1), Matipwili (2), Saleni (1), Mboga (1), Ubena Zomozi (2), Mdaula (3), Kimange (1), Mbwewe (3), Mkange (1), Mkoko (1), Msinune (1), Pingo (1), Diozile (1), Kibaoni (1), Chahua (1), Kihangaiko (1), Kilemela (1), Msigi (1), Mwetemo (1), Mnindi (1), Mindukene (1), Visakazi (1), Tonga (1), Bago (1), Mindutulieni (1) na Changalikwa (1) | Afya | Chalinze DC | Ujenzi wa nyumba nne (4) za watumishi umekamilika, nyumba mbili (2) ujenzi unaendelea katika hatua mbalimbali. Hospitali ya wilaya Msoga (4), Kituo cha Afya Miono (0), Kituo cha Afya Chalinze (0), Kituo cha Afya Msata (0), Kituo cha Afya Kibindu (0), Kituo cha Afya Lugoba (0), Kituo cha Afya Kwaruhombo (0), pamoja na Zahanati za Vijiji vya Vigwaza (0), Kiwangwa (0), Matipwili (0), Saleni (0), Mboga (0), Ubena Zomozi (0), Mdaula (0), Kimange (0), Mbwewe (0), Mkange (0), Mkoko (0), Msinune (1- ujenzi unaendelea), Pingo (0), Diozile (1- hatua ya msingi), Kibaoni (0 Chahua (0), Kihangaiko (0), Kilemela (0), Msigi (0), Mwetemo (0), Mnindi (0), Mindukene (0), Visakazi (0), Tonga (0), Bago (0), Mindutulieni (0) na Changalikwa (0) |
| 4 | Ujenzi wa zahanati 21 katika Vitongoji vya Mtambani (1), Malivundo (1), Magome (1), Pera (1) pamoja na Vijiji vya Kaloleni (1), Mwidu (1), Kitonga (1), Kwazoka (1), Lunga (1), Kisanga (1), Kikwazu (1), Pongwemnazi (1), Mpaji (1), Kunduchi (1), Kwakonje (1), Kikaro (1), Mkwajuni (1), Kipera (1), Makao Makuu (1), Mandera (1) na Makole (1). | Afya | Chalinze DC | Ujenzi wa zahanati umeanza kutekelezwa katika Vitongoji vya Malivundo (1 – hatua ya upigaji rangi),Pera (1 – hatua ya upigaji rangi), Kitonga (1 – hatua ya skimming), Kwazoka (1 – hatua ya upigaji rangi). |
| 5 | Ujenzi wa Vituo vya Afya 5 katika kata za Talawanda (1), Mkange (1), Kiwangwa (1), Vigwaza (1) na Mandera (1) | Afya | Chalinze DC | Ujenzi wa Vituo vya Afya vitano (5) katika kata za Mkange (1 ujenzi unaendelea, OPD imekamilika), Kiwangwa (1 - ujenzi unaendelea OPD na Maternityzimekamilika), Vigwaza (1 - Jengo la wazazi na maabara zimekamilika na imefunguliwa. |
| 6 | Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa Mahututi (ICU) katika Hospitali ya Msoga | Afya | Chalinze DC | Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa Mahututi (ICU) katika Hospitali ya Msoga upo unaendele na umefikia hatuaya skimming. |
| 7 | Ukamilishaji wa Jengo la Utawala katika Hospitali ya Msoga | Afya | Chalinze DC | Ujenzi umekamilika na jengo linatumika |
| 8 | Ujenzi wa zahanati mpya 5 katika mitaa ya Kilimahewa, Kongowe, Muheza, Mkombozi na Lumumba | Afya | Kibaha MC | Zahanati ya Mtaa wa Kilimahewa ujenzi umekamilika na imeanza kutoa huduma, Mitaa ya Kongowe, Muhenza, Mkombozi na Lumumba ujenzi haujaanza |

| NA. | JINA LA MRADI | SEKTA | WILAYA/ HALMASHAURI | HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI JANUARI – MACHI 2026 |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Ujenzi wa majengo 3 ya wagonjwa wa nje katika zahanati za Mtakuja, Miswe na Vikawe | Afya | Kibaha MC | TZS. 40,000,000/= zimepelekwa katika Zahanatiya Mtakuja na TZS. 25,000,000/= zimepelekwa katika katika zahanati ya Miswe ili kuanzisha ujenzi wa majengo husika. Kwa Zahanati ya Vikawe utekelezajibado haujaanza. |
| 10 | Ujenzi wa jengo la upasuaji na wodi yawazazi, katika Kituo cha Afya Mkoani | Afya | Kibaha MC | Ujenzi wa jengo la upasuaji na wodi ya wazazi umekamilika na huduma zinatolewa. |
| 11 | Ukamilishaji wa nyumba 6 za watumishi katika Zahanati ya Mangombela, Mchukwi, Mng'aru, pamoja na Kituo cha Afya Kibiti na Nyamatanga | Afya | Kibiti DC | Ujenzi wa Nyumba tatu kati ya sita. utelekezaji umekamilika ambazo ni Zahanati ya Mng`aru, Mchukwi na Kituo cha Afya Nyamatanga. |
| 12 | Kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji, miundombinu ya vyoo, kichomea taka nashimo la kondo la nyuma kwenye zahanati 5 za Uponda, Mahege, Kibuga na Nyanjati | Afya | Kibiti DC | Vituo vimeshapokea fedha, taratibu za kuanzisha ujenzi zinaendelea katika hatua za manunuzi ikiwemouandaaji wa kutangaza zabuni kwa ajili ya vifaa nafundi kupitia mfumo wa NeST. |
| 13 | Ukarabati wa Zahanati ya Kijiji cha Mlanzi | Afya | Kibiti DC | Ukarababti umekamilika na Zahanati inatoa huduma kwa wananachi. |
| 14 | Ukamilishaji ujenzi wa jengo la wazazi Kituo cha Afya Mjawa na Zahanati ya Bungu | Afya | Kibiti DC | Kituo Cha Afya Bungu, ujenzi unaendelea na upo hatuaya ukamilishaji wa majengo ya awali kwa asilimia 85 |
| 15 | Ukamilishaji wa ujenzi wa Jengo la Maabara – Kituo cha Afya Mjawa | Afya | Kibiti DC | Ujenzi umekamilika, jengo linatoa huduma |
| 16 | Ukamilishaji wa ujenzi wa Jengo la Kuhifadhia Maiti – Hospitali ya Wilaya Kibiti | Afya | Kibiti DC | Ujenzi umeshakamilika, jengo linatoa huduma |
| 17 | Ukamilishaji wa ujenzi wa Jengo la Upasuaji – Hospitali ya Wilaya Kibiti | Afya | Kibiti DC | Ujenzi umekamika na Jengo linatoa huduma kwawananchi. |
| 18 | Ukamilishaji wa ujenzi wa Wodi ya Wanawake na Wanaume – Hospitali ya Wilaya Kibiti | Afya | Kibiti DC | Ujenzi umekamika na huduma inatolewa |
| 19 | Ununuzi wa vifaa tiba ngazi ya zahanati na vituo vya afya | Afya | Kibiti DC | Kwa Robo ya Januari – Machi 2026. Zahanati TZS. 49,000,000.00 na Vituo Vya Afya Tsh 24,000,000.00 zimetumika Kununua Vifaa Tiba. |
| 20 | Ujenzi wa Vituo vya Afya 3 katika Kata zaBungu, Salale na Mtunda | Afya | Kibiti DC | o Ujenzi wa Kituo Cha Afya Bungu upo hatua Plastering,<br>o Ujenzi wa Kituo Cha Afya Nyamisati kata ya Salale upo hatua ya plastering<br>o Ujenzi wa Kituo cha Afya Mtunda umefikia hatuaya Msingi na Jengo moja la Maabara lipo hatua ya kuezeka. |
| 21 | Ujenzi wa nyumba 6 za watumishi wa afya katika kata 6: Chole (Yombolukinga – 1), Marumbo (Chang'ombe B – 1),Msimbu (Kitanga – 1), Kibuta (Bwama – 1), Mzenga (Vilabwa – 1), Vikumburu(Pangalamwingireza – 1) | Afya | Kisarawe DC | o Ujenzi wa nyumba ya mtumishi Zahanati ya Yombolukinga upo hatua ya boma<br>o Ujenzi wa nyumba nyingine kwenye Zahanati za Chango'mbe, Kitanga, Bwama,vilabwa na panga la mwingereza upo hatua ya kusafisha maeneo na ukusanyaji wa vifaa vya ujenzi |

| NA. | JINA LA MRADI | SEKTA | WILAYA/ HALMASHAURI | HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI JANUARI – MACHI 2026 |
|---|---|---|---|---|
| 22 | Ujenzi wa zahanati 17: Chole (Mafumbi, Yombolukinga), Vikumburu (Mtunani, Kitongachole, Koresa), Marui (Titu, Maruingwata), Marumbo (Kikwete, Kitongamango), Maneromango (Kidugalokanga), Kibuta (Mloo), Kisarawe (Kimani), Vihingo (Sangwe), Kazimzumbwi (Visegese, Kifuru), Msanga (Mianzi), Msimbu (Luhangai) | Afya | Kisarawe DC | o Ujenzi wa Zahanati ya Mafumbi, Yombolukinga–umekamilika<br>o Ujenzi wa Zahanati za Titu, Marui Mngw'ata na Kifuru upo hatua ya umaliziaji,<br>o Ujenzi wa Zahanati za Mtunanai, kitonga chole, Koresa, Kikwete, Visegese upo hatua ya Jamvi la Msingi,<br>o Ujenzi wa Zahanati za Mianzi, Kimani upo hatua ya boma.<br>o Ujenzi wa Zahanati za Mloo, Kitongamango, Kidugalo anga, Luhangai – haujaanza. |
| 24 | Ununuzi wa vifaa tiba: Weight Scale with Height (Zahanati ya Mafizi – 2, Zahanati ya Kurui – 2); Trolley Instrument (Zahanati ya Msimbu – 1, Zahanati ya Kiluvya – 1, Zahanati ya Sofu – 1, Zahanati ya Zegero – 1) | Afya | Kisarawe DC | Ununuzi wa vifaa tiba hivyo ulifanyika na kugawiwa kwenye Zahanati kama zilivyoorodheshwa.(100%) |
| 25 | Ujenzi wa zahanati 5 (Baleni, Ndagoni, Kanga, Jibondo) kwa ajili ya kuboresha huduma za afya | Afya | Mafia DC | Zahanati ya Baleni imekamilika na inatoa huduma pamoja na Zahanati ya Jibondo ipo hatua ya upauaji sawa na 67% |
| 26 | Ujenzi wa vituo vya afya 2 (Baleni, Ndagoni) | Afya | Mafia DC | Kwa sasa hivi kituo cha afya Dongo kina jengwa nakimefikia 67% ya utekelezaji |
| 27 | Ujenzi wa vichomea taka 10 katika zahanati | Afya | Mafia DC | Vichomea taka saba vimejengwa |
| 28 | Ukamilishaji wa jengo la mama na mtoto – Hospitali ya Wilaya | Afya | Mafia DC | Jengo limekamilika na linatumika |
| 29 | Ukamilishaji wa Kituo cha Afya Kiegeani | Afya | Mafia DC | Bado hakijakamilika, huduma inatolewa kupitia majengo ya awali ambayo yalishakamilika |
| 30 | Ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti –Hospitali ya Wilaya | Afya | Mafia DC | Jengo limekamilika na linatumika |
| 31 | Ujenzi wa njia za watembea kwa miguu (walkways) – Hospitali ya Wilaya na Vituovya Afya | Afya | Mafia DC | Ujenzi wa njia kwa Kituo cha Afya Kiegeani umefikia 80%, Kituo cha Afya Kirongwe na Hositali ya Wilayaujenzi haujaanza. |
| 32 | Ukamilishaji wa zahanati 27: Hoyoyo, Bigwa, Kibudi, Nyamato, Tipo, Funza, Luzando, Tambani, Kikundi, Kizomla, Lugwadu, Mkokozi, Mwanzega, Ngarambe, Mipeko, Kikoo, Kimanzichana Kaskazini, Kiparang'anda "B", Kibululu, Vianzi/Kisegese, Kondomwelanzi, Dondo, Mihekela, Kigobedi, Kolagwa, Uboreshaji wa Zahanati ya Bupu | Afya | Mkuranga DC | o Ujenzi wa Zahanati za Hoyoyo, Bigwa, Nyamatotipo, Kikundi, Kizomla, Lugwadu, Mkokozi, Kiparang'anda B, Kibululu, Mipeko, Vianzi Kisegese, Dondo, Kondomwelanzi, Kibudi, Kigobedi na Zahanati ya Bupu umefikia hatua ya ukamilishaji na ujenzi unaendelea.<br>o Ujenzi wa Zahanati za Funza, Luzando,Tambani, Kikoo,Mihekela, Kolagwa, Ngarambe, Lugwadu, Mkokozi na Mwanzega umekamilika kwa 100% |

| NA. | JINA LA MRADI | SEKTA | WILAYA/ HALMASHAURI | HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI JANUARI – MACHI 2026 |
|---|---|---|---|---|
| 33 | Ujenzi wa zahanati 50: Matanzi, Mkenge, Nyangunguti, Mamdimpera, Mamdimkongo, Kibewa, Kimbwanindi, Mkuchembe, Kimanzichana Kusini, Kilimahewa Kaskazini, Kise, Kibesa, Kerekese, Mavunja, Kipera, Mitaranda, Malenda, Mkola, Mpimio, Misasa, Sangalani, Mponga, Msonga, Mtongani, Nyamihimbo, Kisayani, Kigoda, Kibunguchana, Mkerezange, Tungi, Dundani, Mkuranga, Mgawa, Picha ya Ndege, Yavayava, Kitonga, Kinene, Tengelea (Gogo), Mikera, Mingombe, Mkuruwili, Kilimahewa Kusini, pamoja na vijiji vingine vilivyopo kwenye mpango (idadi 50) | Afya | Mkuranga DC | o Ujenzi wa Zahanati zinazoendelea kwa sasa ni Kimbwanindi, Kimanzichana kusini, Kilimahewa Kaskazini, Kise, Kerekese, Mponga, Msonga,Sangalani, Dundani, Mkuranga, Picha ya Ndege, Yavayava, Tengelea(Gogo), Mikere na Mingombe. Ujenzi umefikia hatua mbalimbali za utekelezaji.<br>o Ujenzi wa Zahanati zilizokwenye mpango na bado hazijapokea fedha ni Mkuruwili, Kilimahewa Kusini, Kitonga, Kinene, Mtongani, Nyamihimbo,Kisayani, Kigoda, Kibunguchana, Mkerezange, Tungi, Mavunja, Kipera, Mitaranda, Malenda, Mkola, Mpimio, Misasa, Kibesa, Mkuchembe, Kimanzichana Kusini, Mkenge, Nyangunguti, Mamdimpera, Mamdimkongo na Kibewa. |
| 34 | Ujenzi wa vituo 12 vya afya: Kipala Mpakani, Ngunguti, Makumbea, Mwanambaya, Bupu, Njianne, Lukanga, Vianzi, Mipeko, Tambani, Mwarusembe, Shungubweni | Afya | Mkuranga DC | o Ujenzi wa majengo ya awali kwa Vituo vya Kipalampakani, Ngunguti, Makumbea na Shungubweniyamekamilika kwa 100%.<br>o Kituo cha Afya Mwanambaya kimepokea fedha kwa majengo ya awali, ujenzi haujaanza<br>o Vituo vilivyokwenye mpango na bado havijapokeafedha ni Njianne, Lukanga, Vianzi, Mipeko, Tambani na Mwarusembe |
| 35 | Ujenzi wa nyumba 10 za Waganga Wafawidhi: Kisiju Pwani, Kitomondo, Sotele, Mihekela, Funza, Kolagwa, Tengerea, Msorwa, Nyamato, Makumbea | Afya | Mkuranga DC | o Ujenzi wa nyumba nne (4) za Waganga Wafawidhi zilizokamilika kwa 100% [Funza, Kitomondo, Sotele, na Nyamato tipo].<br>o Ujenzi wa nyumba mbili (2) za Waganga unaendelea katika Zahanati za Kisiju Pwanina Mihekela<br>o Ujenzi wa nyumba nne (4) za Waganga Wafawidhi zilizo kwenye mpango: Kolagwa, Tengerea, Msorwa, Makumbea |
| 36 | Upanuzi wa miundombinu Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga | Afya | Mkuranga DC | Upanuzi wa miundombinu ya Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga:<br>o Ujenzi unaendelea kwa ujenzi wa Jengo la matibabu la watoto wachanga (NICU), Jengo la upasuaji na ukarabati wa jengo la matibabula watoto wachanga.<br>o Ujenzi wa jengo la matibabu ya waraibu wa dawaza kulevya limekamilika kwa 100% |
| 37 | Ujenzi wa zahanati mpya 5: Kikobo, Shauri Moyo, Mihiru, Mtanange na Bwawani | Afya | Rufiji TC | Utekelezaji bado haujaanza, isipokuwa kwa Zahanatiya Mihilu fedha imeshatengwa kwa mwaka wa fedha 2025/26 – Tsh 205,000,000 ujenzi upo hatua za awali. |
| 38 | Ujenzi wa vituo vya afya 4: Nambunju, Umwe, Chumbi na Mohoro | Afya | Rufiji TC | Ujenzi unaendelea,<br>o Kituo cha Afya Nambunju kimefikia hatua yaplastering<br>o Kituo cha Afya Mohoro, ujenzi umefikia hatuaya upigaji wa rangi.<br>o Kituo cha Afya cha Umwe, ujenzi umefikia hatuaya umwagaji wa jamvi la juu,<br>o Ujenzi wa Kituo cha Afya Chumbi, ujenzi upohatua ya uchimbaji wa Msingi |

| NA. | JINA LA MRADI | SEKTA | WILAYA/ HALMASHAURI | HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI JANUARI – MACHI 2026 |
|---|---|---|---|---|
| 39 | Ukamilishaji wa zahanati 7: Nyawanje, Kipoka, Kikongono, Nyandakatundu, Kindwitwi, Kitapi na Kifuru | Afya | Rufiji TC | o Ujenzi wa Zahanati za Nyawanje, kipoka, kikongono, Nyandakatundu, Kindwitwi na kitapi,ujenzi unaendelea katika hatua mbalimbali kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026<br>o Ujenzi wa Zahanati ya Kifuru umetengewa TZS.80,000,000 na kwa sasa umefikia 77%. |
| 40 | Ufungaji wa mfumo wa GoTHoMIS katika zahanati: Nyandakatundu, Ngorongo Magharibi, Mgomba Kusini, Tapika, Ruwe, Kindwitwi, Mtanza, Kitapi, Mbambe, Nambunju na Ndundunyikanza. | Afya | Rufiji TC | Ufungaji mfumo wa GoTHoMIS umeshatekelezwakwa vituo vyote katika Halmashauri ya Mji wa Rufiji. |
| 41 | Ujenzi wa hospitali kubwa ya kanda Kataya Mbwara (Nyamwage) | Afya | Rufiji TC | Eneo la takribani heka 53 lime tengwa na Kijiji cha Nyamwage. Timu ya Wizara ya Afya ilishafika kwenyeeneo lililotengwa kwa ajili ya ukaguzi . |




*Kituo cha Afya Kipala Mpakani, Mwandege - Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*



Kituo cha Afya Bungu Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti




Zahanati ya Kilimahewa Manispaa ya Kibaha

## 3.5. SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

### 3.5.1. Utoaji wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

**Ibara ya 33 (e) Kuongeza utoaji wa mikopo ya asilimia 10; Mkoa utasimamia na Kuhakikisha kwamba Halmashauri zote za Mkoa wa Pwani zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo kwa mujibu wa Sheria ili kuwezesha vijana na makundi mengine katika jamii kupata mikopo isiyo na riba.**

Mwaka 2025/26, kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Halmashauri zilipaswa kuchangia jumla ya TZS. **6,955,238,083.52** kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kulingana na Mapato yaliyokusanywa. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya TZS. **5,294,677,586.29** zimechangiwa sawa na asilimia **76.12**. Katika utoaji wa mikopo 2025/26 TZS. **11,598,027,093.00** (Wanawake TZS. **5,334,210,205.00**,

Vijana TZS. **5,780,080,376.00**, Watu wenye ulemavu TZS. **483,736,012.00**) zimetolewa kwa makundi ya Wanawake **670**, vijana **389** na watu wenye ulemavu **77**.




*Utoaji mikopo ya asilimia kumi katika Manispaa ya Kibaha*





*Baadhi ya Magari ya Vikundi vya Vijana waliokopeshwa mikopo ya asilimia kumi katika Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo na Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

### 3.5.2. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III)

**Ibara 33 (f): Kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa kunusuru kaya masikini kwa kuhakisha miradi ya kupunguza umasikini kupitia TASAF inakuwa endelevu;-**

Mkoa wa Pwani umepata fursa ya kuanza utekelezaji wa zoezi la utambuzi na uandikishaji wa kaya zilizopo katika maeneo yenye hatari ya kuathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi lililoanza kutekelezwa tarehe 29 Desemba, 2025 katika Halmashauri tano (5) ambazo ni Chalinze, Kibaha DC, Kibiti, Mkuranga na Kisarawe. Katika zoezi hilo kaya 29,801 zilitambuliwa katika kata 45 zenye Vijiji 232 kupitia mikutano ya Vijiji na kufikia Machi, 2026 Kaya 23,754 zimesajiliwa sawa na asilimia 79.71. Mchanganuo unaonekana kwenye Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10: Mchanganuo wa Kaya Zilizo katika Maeneo yenye hatari ya kuathiliwa na Tabia ya Nchi**

| Na | Halmashauri | Kata | Vijiji/ Vitongoji | Kaya Zilizotambuliwa | Kaya Zilizosajiliwa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Chalinze | 1 | 8 | 1,934 | 1,748 | 90.38 |
| 2.. | Kibaha | 1 | 7 | 306 | 293 | 95.75 |
| 3. | Kibiti | 1 | 7 | 809 | 762 | 94.19 |
| 4. | Kisarawe | 17 | 85 | 8,245 | 7,607 | 92.26 |
| 5.. | Mkuranga | 25 | 125 | 18,507 | 13,344 | 72.10 |
| | **JUMLA** | **45** | **232** | **29,801** | **23,754** | **79.71** |

Lengo la utekelezaji huu ni hatua ya kimkakati ya Serikali kuandaa daftari la Kaya Maskini ambazo zinaweza kuingia kwenye umaskini uliokithiri endapo mabadiliko ya tabia nchi na Maafa ya asili yatatokea, takwimu hizi zitawezesha kutoa msaada wa haraka wakati wa majanga kama ukame na mafuriko pamoja na kuwezesha kaya masikini kupata huduma za afya bure ili kupunguza changamoto za kushindwa kupata matibabu na vifo.

Takwimu za uandikishwaji wa kaya zilizopo katika hatari za kupatwa na majanga ya asili kufikia Machi, 2026.



*Mwezeshaji akitoa elimu kwa Wananchi wa Kijiji cha Mengwa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe wakati wa zoezi la utambuzi wa kaya lililofanyika kijijini hapo tarehe 18/02/2026*

## 3.6. UKUSANYAJI WA MAPATO

### 3.6.1. Ukusanyaji Wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania Mkoa Wa Pwani (TRA – Pwani)

Katika mwaka wa fedha 2025/2026 hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Pwani ilikadiria kukusanya jumla ya TZS.. 189,645,661,196.21 kutoka katika Kodi za ndani na Forodha ambapo jumla ya TZS.. 216,029,059,888.91 zimekusanywa sawa na asilimia 113.91. Mchanganuo wa makusanyo hadi kufikia Machi, 2026 unaonekana katika Jedwali Na. 11.

**Jedwali Na. 11: Mchanganuo wa Makusanyo ya Kodi za Mapato ya TRA hadi kufikia Machi, 2026**

| Na. | Chanzo | Malengo | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kodi za Ndani | 80,921,548,051.80 | 104,125,698,309.01 | 128.67 |
| 2 | Kodi ya Forodha | 108,724,113,144.41 | 111,903,361,579.90 | 102.92 |
| | **JUMLA** | **189,645,661,196.21** | **216,029,059,888.91** | **113.91** |

### 3.6.2. Mapato ya Ndani ya Halmashauri

**Kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha makusanyo ya mapato katika vyanzo vilivyopo ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.**

Mkoa umendelea kupata mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa mapoto kupitia Halmashauri ambapo mwaka 2025/26 Halmashauri zimeidhinishiwa makisio ya TZS. **87,957,600,000.00** ikiwa ni ongezeko la TZS. **14,503,152,400.00** kutoka TZS. 73,454,447,600.00 mwaka wa fedha 2024/25 sawa asilimia 19.74. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 jumla TZS. **92,419,674,096.1**6 zimekusanya sawa na asilimia 105.07. Mchanganuo wa makusanyo hadi kufikia Machi, 2026 unaonekana kwenye Jedwali Na. 12.

**Jedwali Na. 12: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri hadi kufikia Machi, 2026**

| NA. | HALMASHAURI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | MAPATO HALISI YALIYOKUSANYWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kibaha Manispaa | 13,895,046,000.00 | 20,372,380,400.54 | 146.62 |
| 2 | Bagamoyo | 8,452,808,000.00 | 6,760,647,889.92 | 79.98 |
| 3 | Mafia | 3,792,737,000.00 | 2,377,237,112.51 | 62.68 |
| 4 | Kisarawe | 5,807,601,000.00 | 5,270,249,833.68 | 90.75 |
| 5 | Kibaha | 5,087,869,000.00 | 11,378,657,569.01 | 223.64 |
| 6 | Rufiji | 6,781,952,000.00 | 4,939,603,219.67 | 72.83 |
| 7 | Mkuranga | 17,325,855,000.00 | 16,474,464,277.72 | 95.09 |
| 8 | Chalinze | 22,243,578,000.00 | 21,986,157,888.74 | 98.84 |
| 9 | Kibiti | 4,570,154,000.00 | 2,860,275,904.37 | 62.59 |
| | **JUMLA** | **87,957,600,000.00** | **92,419,674,096.16** | **105.07** |

## 3.7. SEKTA YA MICHEZO

### 3.7.1 Kudumisha Utamaduni wa Taifa, na Kukuza Sanaa na Michezo

**Ibara 42. (f) – (g): Kutenga, kulinda na kuendeleza angalau kiwanja kimoja cha michezo chenye hadhi ya kitaifa pamoja na Kujenga na kukarabati viwanja 14 vya michezo;**

Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze inaendelea na ujenzi wa uwanja wa kisasa wa mpira katika Kata ya Msonga. Mradi huo umeanza kutekelezwa 1 Oktoba, 2025 ambapo mwaka 2025/26 TZS. **2,253,325,510.29** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji. Mradi huo unaotekelezwa na Mkandarasi Monmar and son company LTD. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 52 na unatarajiwa kukamilika tarehe 1 Agosti, 2026.

Aidha, Halmashauri ya manispaa ya Kibaha imetenga eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 126,101 katika eneo la Mitamba kata ya Pangani kwa ajili ya kujenga kiwanja cha mpira chenye hadhi ya kimataifa.



*Pichani ni Mhe. Mkuu wa Mkoa Pwani pamoja na Kamati ya siasa Mkoa wa Pwani walipo tembelea na kufanya ukaguzi katika mradi wa Ujenzi wa Uwanja, Kata ya Msoga - Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze.*

## 3.8. SEKTA YA UTAWALA BORA NA UTAWALA WA SHERIA

**Ibara ya 43; (b): Kuwashirikisha wananchi katika ulinzi wa mali na jamii zao;**

Serikali imeendelea kuwashirikisha wananchi katika ulinzi wa jamii kupitia uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya ulinzi shirikishi kwenye kila kata pamoja na kutoa elimu ya usalama kwa jamii. Hali ya Usalama katika Mkoa imeendelea kuwa tulivu japokuwa mara chache matukio madogomadogo yanajitokeza na kudhibitiwa na vyombo vya Usalama.

**Ibara ya 43; (c): Kuzuia rushwa na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wote wanaothibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa na uvunjifu wa maadili;**

Katika kupambana na Rushwa, Ofisi ya TAKUKURU Mkoa katika kipindi cha januari hadi Machi, 2026 imefanikiwa kutoa elimu na mafunzo ya kuzui na na kupambana na rushwa kwa jamii kwa njia mbalimbali ikiwemo Semina 51, Mikutano ya Hadhara 24, Maonyesho 4 na Vipindi vya Redio 8. Aidha, Klabu za Rushwa 158 katika shule za msingi na sekondari zimeimarishwa.

Taasisi imefanya ukaguzi wa miradi **53** ya maendeleo yenye thamani ya TZS. **1,613,175,779,123.80.** Kati ya miradi hiyo **17** ilikuta na dosari ambapo wasimamizi wa miradi wameagizwa kurekebisha mapungufu yaliyobainika na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa ajili ya uhakiki.

**Ibara ya 43; (d): Kuimarisha uwajibikaji miongoni mwa Viongozi na Watumishi wa Umma**

Serikali ya Mkoa imeendelea kuhakikisha Watumishi wanapata mafunzo ya maadili ya Utumishi wa Umma na kuwasimamia kikamilifu katika masuala ya uwajibikaji, uwazi, na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Kwa kipindi cha Disemba, 2025 hadi Machi, 2026, Mkoa umepokea jumla ya malalamiko 35 yakiwemo 19 ya kiutawala na 16 ya ardhi. Kati ya malalamiko hayo malalamiko 7 yameshashughulikiwa na kumalizika na malamiko 27 yanaendelea yakihusisha vyombo vya Sheria.

Aidha, mifumo ya ndani ya kushughulikia malalamiko ya wananchi imeendelea kuimarishwa kwa kutenga siku (1) ya kupokea na kusikiliza kero na Malalamiko mbalimbli ya Wananchi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya. Aidha, Viongozi wameendelea kufanya mikutano ya Kata kwa Kata kwa ajili ya utatuzi wa changamoto na kero za Wananchi.

## 4.0 HITIMISHO

Mkoa wa Pwani unaendelea kudumisha Amani, Utulivu, Umoja na Mshikamano ili kujenga mazingira yenye Utulivu na Rafiki kwa wananchi na Serikali kuendelea na shughuli zao za Kijamii, Kiuchumi na Maendeleo bila vikwazo vyovyote.

Serikali itaendelea kusimamia na kutekeleza Miradi kwa Weledi, Uadilifu na Ufanisi ili kuondoa kero za wananchi na kuboresha maisha yao. Kwa kuwa Mkoa wa Pwani ni Mkoa wa Kimkakati katika Sekta ya Viwanda na Uwekezaji, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kupata wawekezaji Makini na Mahiri. Uwekezaji utasaidia kuongeza Ajira kwa Vijana wetu, Vijana wetu kujifunza Ujuzi na Teknolojia mbalimbali za kisasa, Serikali itapata Kodi na fedha za Kigeni, Wananchi watapata kwa urahisi mahitaji yao ya bidhaa zitakazozalishwa na Wananchi kunufaika na huduma kwa Jamii (Corporate Social Responsibility)

Ili malengo hayo yaweze kutimia Serikali itahakikisha inaendelea kuwa mahusiano mazuri na bora na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili kuendelea kutekeleza Ilani ya Chama kwa Kasi na Ufanisi mkubwa. Hii itahakikisha Wananchi wanaendelee kukiamini Chama kupitia Ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2025 - 2030.

***"KIDUMU CHAMA CHA MAPINDUZI"***



ABUBAKAR M. KUNENGE
**MKUU WA MKOA PWANI**

CHAMA CHA MAPINDUZI

# KAZI NA UTU

## TUNASONGA MBELE